Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 73 No. 168 | JUMADIUL-AWWAL1433AH | MACHI 2012 | AMMAN 1391 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu. ***(An-Nisaa 4:2).***

AULIZAYE ATAKA KUJUA:
Uhai wa Islam unapatikana wapi?

Na Mwandishi wetu

Dunia imo katika masumbuko makubwa ya kutafuta nusura. Taifa kubwa duniani kwa utajiri na silaha Marekani, wao ndio chimbuko la maumivu tuliyonayo. Umoja wa mataifa uko chini ya bawa la Marekani. Umoja huu haufurukuti bila ya rukhusa ya Marekani. Njia pekee iliyobaki ni kugonga kwenye mlango wa Islam na tuone inatupatia ufumbuzi gani wa masumbuko yetu haya.

Kwa mnasaba wa kuleta uhai wa Islam, Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani anatufungulia hazina ya Islam, kwani kila ugonjwa una dawa. Kiongozi huyo hivi karibuni alifafanua jambo hili vya kutosha.

Huzur (atba) alielezea hadithi ya Mtume Mtukufu (saw) isemayo Mungu Atawatuma Mujaddidin, au Wahuishaji, kwa ajili ya kuhuisha Islam katika kila karne. Mara kwa mara maswali yanaendelea kuulizwa kuhusiana na hadithi hii, swali kama hili limeulizwa pia katika kipindi cha Waqf-e-Nau siku chache zilizopita. Maswali haya si mapya kwa vile yameshawahi kuulizwa katika kipindi cha Makhalifa wetu waliotangulia ambao waliyajibu sawa na haja.

Ukweli ni kwamba maswali haya huulizwa kwa uchimvi kama ilivyotokea wakati wa Khalifatul Masih III (rh). Lakini kila wakati watu wanapokusudia kuleta husuda Mungu haachi kuwazuia kwa mkono wake wenye nguvu.

Huzur (atba) akaeleza kwamba Masihi aliyeahidiwa amefafanua wazi kabisa kwamba, kwa mujibu wa bishara hii, kila haja itakapozuka Allah Ataleta njia kwa ajili ya kuwahuisha Waislam, kuondoa upotovu ulioingizwa baadae katika dini na kurejesha mafundisho sahihi ya imani. Kwa mnasaba huu Mujaddid walikuja ili kutimiza lengo hilo.

Huzur (atba) akaendelea kusema; hii ni milenia ya mwisho kwa ulimwengu na kwa ajili ya kipindi hiki Masihi aliyeahidiwa (as)

Endelea uk. 3



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a

Msikiti wafunguliwa mjini Arusha

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Tarehe 02/02/2012 jiji la Arusha lilikuwa katika shamra shamra za ufunguzi wa Msikiti wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Ufunguzi huo ulifanywa na Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry na kuhudhuriwa na wageni wengi waliotoka sehemu mbalimbali hapa nchini.

Akifungua Msikiti huo, Sheikh Tahir alifafanua kwa uwazi falsafa ya Misikiti sawa na mafundisho ya dini tukufu ya Islam. Alisema ya kwamba Misikiti ni nyumba ya Mwenyezi Mungu na mtu yeyote ana haki ya kufanya ibada isipokuwa mambo yote yanayoambatana na ushirikina hayaruhusiwi katika nyumba hiyo. Alisema ya kwamba Msikiti ni kielelezo cha usawa wa binadamu, kwani Msikitini haitizamwi hadhi au nafasi ya mwaminio katika jamii. Hivyo alitoa mwito kwa watu wote wawe huru katika kutumia nyumba hiyo ya Mwenyezi Mungu kwani shabaha kubwa ya ujenzi wa Msikiti huo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu.

Sheikh Tahir pia alitoa maelezo mafupi kuhusu sehemu hiyo, na akasema ya kwamba sehemu hiyo ilitolewa waqfu na Mwanajumuiyya Marehemu Alhaji Ahmad Okash Haruni ambaye alikuwa na jazba kubwa sana katika kuhubiri na kuipenda Jumuiyya Ahmadiyya.

Maisha ya simba huyu wa

Endelea uk. 2



Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood akiwa kwenye picha ya pamoja na Mstahiki Meya (katikati) wa jiji la Arusha. Kulia ni Sheikh Khawaja Muzaffar ambaye anasimamia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

Ndoa ya utulivu - Pepo ya Dunia

Na Amtul Noor Daud sahiba - Sadr Lajna Imaillah, Canada:

Katika Qur'an Tukufu, Allah Anasema; "Enyi watu! Mcheni Mola wenu Ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu". (4:2)

Katika aya niliyoitaja, Allah Mwenye Enzi Anatuamuru kuifanya Taqwa kuwa msingi wa mahusiano yetu yote. Ikiwa tutakuwa na daraja la juu la Taqwa ndani yetu, tutapata uwezo wa kutendeana baina yetu kwa heshima, adabu, mapenzi na haki. Matokeo yake, hii itapelekea kupatikana utulivu majumbani na katika familia au kwa maneno mengine "pepo duniani".

Mtume Mtukufu (saw) alichagua aya hii ya Qur'an Tukufu katika kurasimisha ndoa ya Kiisla. Kuna umuhimu wa kipekee kuelewa kuwa katika fungamano la ndoa, kutimiza tu matamanio ya mtu na kuzinywesha hisia zake sio kusudio hasa, bali lengo ni kujenga mazingira ya utulivu yenye uaminifu, heshima na mapenzi baina ya wanandoa. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba mahusiano yote baina ya wanandoa yaakisi msingi imara wa Taqwa na kwamba hali ya kumwogopa Allah Mwenye Enzi iwepo nyoyoni mwao wakati wote.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) ametukumbusha pia juu ya dhumuni hili, amesema katika moja ya hotuba zake; "Wote waume na wake lazima waangalie kwamba Taqwa inadumishwa, maombi yatumike katika kustawisha mahusiano, heshima wapewe

Endelea uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Mabadiliko na Tujisahihishe

Historia ya nchi yetu imetawaliwa kwa kiwango kikubwa na dhana mbili; 'MABADILIKO na TUJISAHIHISHE', ni dhana hizi mbili ambazo zimelisaidia taifa hili liwe kama lilivyo hivi leo. Tumeruhusu mifereji hii miwili itiririke mwanana bila kuleta bughuda yoyote katika nchi na hiyo ndiyo imekuwa siri ya mafanikio yetu.

Tanganyika ilitawaliwa na Mjerumani, na baadae ikatawaliwa na Mwingereza.

Hatimaye nchi hii ikajipatia uhuru. Na katiaka harakati hizo za kuleta maendeleo, mabadiliko makubwa yalifanyika. Yawe ni mazuri au mabaya. Machifu waliondolewa, lugha ya Kiingereza ikawa lugha ya pili nchini, elimu ikawa kwa ajili ya kuwatumikia wakulima na wafanyakazi. Hayo ni mabadiliko makubwa ambayo yalifanywa na nchi hii na kuisaidia kupata jina si tu katika bara la Afrika, bali katika sehemu nyingine za dunia.

Kama taifa bila shaka hatukuwa na mkamilifu mkubwa. Kwa kumaizi jambo hilo tukajiwekea utamaduni mwingine wa kujisahihisha. Nchi yetu imejijengea utamaduni wa kutambua kuwa wanaoishi humu ni binadamu na sio malaika. Ada ya binadamu siku zote ni kukosea, na anapokosea anafanya mabadiliko.

La kufurahisha sana katika nchi yetu hii, ni kwamba kila tulipofanya makosa tulifanya haraka kujisahihisha. Hii ni alama ya uungwana na kukiri utu wetu. Mwaka 1967 kwa mfano sawa na azimio la Arusha -nyumba nyingi zilizokuwa zimepangishwa zilitaifishwa. Eti zikapewa jina 'mali ya uma'. Nakumbuka hata nyumba zilizokuwa za mashirika ya dini zilitaifishwa. Hatua hii ilimfanya Maulana Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry ambaye alikuwa ni Amir na Mbashiri wa Tanzania amwandikie barua Rais Julius Kambarage Nyerere ili arudishe nyumba za dini.

Kwa kufuata utamaduni ule ule wa kujisahihisha, nyumba hizo zilirudishwa. Wamekuwepo pia watu ambao kwa kujuana au kwa kuwa na jina wameweza kupata nyumba zao. Lakini wengi mpaka hivi leo wanaendelea kunung'unika katika nafsi zao.

Ni lazima tukumbuke kuwa katu nchi haipati baraka na wala haiendelei inapokuwa na baadhi ya raia ambao wamedhulumiwa. Hapana shaka kutaifisha nyumba zile ilikuwa ni dhuluma kubwa sana. Tunazo taarifa za watu waliojinyima ili kujenga nyumba hizo. Ni kosa jingine kubwa kufikiria kuwa nyumba hizo zilikuwa ni za kabila fulani au watu wa rangi fulani. Hao wote ni watanzania bila kujali kabila, rangi au dini. Na moja ya sifa ya nchi hii ni kuamini kwamba binadamu wote ni sawa na kutojali kabisa masuala ya dini, taifa, kabila au rangi.

Kilio cha mtu aliyeonewa kinakwenda moja kwa moja kwenye baraza la Mwenyezi Mungu. Tufanye jitihada kubwa ya kurekebisha makosa yetu haya. Wale waliotaifishiwa nyumab zao ni vikongwe wasio mbele wala nyuma. Kama jana ilikuwa dhambi kuwa na nyumba ya kupangisha kwa hivi sasa dhambi hiyo imefutwa. Tunaomba tujisahihishe katika hilo.

Jambo jingine ambalo linasononesha moyo, ni kuwaona wazee wetu waliokuwa wakifanyia Jumuiyya ya Afrika Mashariki, wakitangatanga huku na kule, wakipewa ahadi asubuhi na jioni na yote hayo waliyoahidiwa hakuna hata moja lililotekelezwa. Nchi inawezaje kupata baraka iwapo wale waliolitumikia taifa hili wanapigwa mithili ya mpira? Kwa nini tusifikiri ya kwamba baadhi ya matatizo yetu nchini humu yanatokana na manung'uniko yanayotokana na wazee wetu hawa? Nchini Kenya wazee hao wamekwisha lipwa na huko Uganda mpaka wamekwisha sahau juu ya pesa hizo. Ni aibu kubwa kwa taifa la Tanzania linaloheshimika kwa kuheshimu haki za binadamu likijikuta katika tope hilo linalonuka.

Bila ya kujisahihisha maendeleo ya binadamu hapana shaka yatachelewa sana. Tunaloweza kwa hivi sasa ni kujipaka rangi hiyo ya kujisahihisha kwani tuna matumaini makubwa itatusaidia tutoke katika ukungu huu tuliyomo hadi tunyeshewe na mvua ya neema.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Msikiti wafunguliwa mjini Arusha

Kutoka uk. 1

Arusha Alhaji Ahmad Okash Haruni mzaliwa wa Arusha Mjini, mama Muarusha na Baba Msomali yanatukumbusha umuhimu wa kuwa jasiri katika kupambana na matatizo hususan yanayohusu masuala ya imani.

Alhaji Okash alikuwa shujaa asiye hofu chochote isipokuwa Mola wake. Na kila alipokwisha iona kweli basi hata ufanye nini Okash harudi nyuma. Okash ni mtu aliyekuwa na nafasi yake, mkulima mashuhuri huko Boma la ng'ombe, Thai, Olonyosungu -Arusha. Ni mashamba haya yaliyomfanya kuwa na hali nzuri ya maisha na kipato cha kutosha.

Mwalimu Shabani Shoo yule Mwalimu mwepesi katika mahubiri na uuzaji wa vitabu vya dini, alipokuwa anatembeza vitabu alimuuzia Alhaji Okash Qur'an Tukufu na gazeti la Mapenzi ya Mungu. Kwa upande wake Alhaji Okash aliisoma kwa makini tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiswahili iliyotolewa na Jumuiyya ya Waislam Wa Ahmadiyya na gazeti la Mapenzi ya Mungu. Toka apate Qur'an Tukufu hiyo katika Kiswahili alianza kuagiza moja kwa moja gazeti la Mapenzi ya Mungu. Yote aliyoyasoma yalimuingia akilini na akawaeleza utamu huo aliokuwa ameugundua kwa Masheikh wake. Masheikh wake walipiga kelele na kumtaka aache kabisa kusoma maandiko ya Makadiani. Alhaji Okash tayari alikwisha ona kweli, nani angethubutu kumrudisha nyuma?

Kuondoa mzizi wa fitina, aliwaalika Masheikh wa pande mbili - Wa Ahmadiyya na Sunni, ili kila mmoja atetee itikadi yake. Hakuna Msomali yeyote wa Mjini Arusha aliyebaki nyumbani. Masheikh wenye vilemba vikubwa vikubwa huku wamebeba vitabu vyao, walikusanyika uwanjani ilipo nyumba ya Alhaji Ahmadi Okash. Umati mkubwa wa watu ulihudhuria na Okash akatangaza ya kwamba yeyote atakayeshinda basi mimi nitafuata huko aliko. Wataalamu wa Jumuiyya ya Ahmadiyya walitoa maelezo yao, wakionesha na kutoa ushahidi juu ya kuendelea kwa utume, wakathibitisha kutoka kwenye Qur'an Tukufu juu ya kifo cha Nabii Isa (as) na wakahakikisha ukweli wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) kwamba yeye ni Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi.

Alhaji Okash aliendelea kusikiliza dhifa hiyo ya kisomi huku akitabasamu, na kuwahimiza Maulamaa wa Kisunni wajibu hoja hizo. Bila woga alisimama baada ya mjadala na kusema ya kwambal, "ndugu zangu mimi naondoka, nakwenda kujiunga na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya au nipeni sababu kwa nini nisijiunge". Masheikh wake walikaukiwa mate na wakawa hawana la kusema. Hivyo kadamnasi mwaka 1962 Alhaji Ahmadi Okash Haruni akajiunga na Jumuiyya ya Waislam Wa Ahmadiyya.



Al-Hajj Ahmad Okash Haruni - Ahmadiyya mshuhuri wa mjini Arusha akiwa na baadhi ya Wanajumuiya wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Ilizuka fitina kubwa sana mjini Arusha. Jitihada kubwa ya kumtenga ilifanyika, lakini yeye aliendelea kushika kamba ya Mwenyezi Mungu, bila ya hofu yoyote akaendelea kusimamisha sala na hususan sala za Tahajjudi. Alhaji Ahmadi Okash hadi hivi leo anakumbukwa kama mtu aliyekuwa mkarimu na wenye huruma sana. Alijitolea sana katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa mfano alianzisha Madrasa ambayo alikuwa akimlipa Mwalimu na hakuna kitu alichokipenda sana kuliko mahubiri.

Kwa moyo mkunjufu alimpa Mwalimu Shabani Shoo usafiri ili aweze kwenda huku na huko ili kuhubiri ufikaji wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Alitoa shamba lake na kuipatia Jumuiyya na nyumba hii ambayo imekarabatiwa na kuwa Msikiti.

Jazba yake ya mahubiri ilikuwa kubwa sana, kila aliyefika nyumbani kwake jambo la kwanza alililomueleza ni kwamba Masihi amekwishafika na hivyo asichelewe kujiunga naye. Alhaji Ahmadi Okash alikwenda mbali zaidi katika mahubiri na akaweka katika kanda baadhi ya vitabu kwa mfano Mambo, na kuvipeleka hadi sokoni kwenye gari lake na akafungua kwa sauti ili watu wasikilize ukweli. Ni yeye pia ambaye alifanya mipango ili Sheikh Muhammad Abdi aweze kwenda Pakistani kwa ajili ya mafunzo ya Usheikh.

Alhaji Ahmad Okash alikuwa ni mfano wa kutanguliza mbele dini mbele ya kila kitu. Na mapenzi yake kwa Jumuiyya yalikuwa ni makubwa sana kiasi ya kwamba kila mtaa aliopita mjini Arusha walikuwa wanasema; "huyoo Kadiani". Lakini hawakudiriki kusema kwa sauti kubwa kwa sababu wengi walikuwa wanafadhiliwa na yeye, kwani licha ya imani Mwenyezi Mungu Alimpatia kipato kizuri na roho ya ukarimu wa kutoa.

Kutokana na ukarimu wake huo, watu wa mjini Arusha hawakuwa na njia isipokuwa kumchagua kuwa Diwani wao. La ajabu ni kwamba wao ndio waliomuomba tena kwa unyenyekevu ili awatumikie kama Diwani. Na kweli kazi kubwa ilifanywa na Diwani Alhaji Ahmadi Okash. Mabadiliko makubwa yalifanyika mjini Arusha. Na ni yeye aliyetoa wazo ule uwanja wa Arusha uitwe 'Sheikh Kaluta Amri Abedi'.

Alhaji Ahmadi Okash Haruni bado anakumbukwa kwa mapenzi makubwa mjini Arusha. Wakati wa ufunguzi wa Msikiti wa Arusha tafrija nzima ya sherehe hiyo iligharamiwa na familia yake. Maisha ya Alhaji Ahamdi Okash Haruni ni alama ya ufaulu kwani daima 'Wamchao Rahman ndio wenye mwisho mwema'.

Hata hivyo sherehe za ufunguzi wa Msikiti zilifanikiwa kuua ndege wawili kwa jiwe moja; mara baada ya ufunguzi wa Msikiti ulifanyika Mkutano kuhusu Amani ambao ulihudhuriwa na viongozi wa dini nao wakaeleza mafundisho yao kuhusu suala zima la Amani. Meya wa jiji la Arusha pia alikuwepo.

Katika hotuba yake Meya huyo wa Arusha alitoa shukrani kwa mwaliko huo na akasisitiza ya kwamba hakuna suala lililo nyeti na zito katika nchi yetu kama Amani. Alisema ya kwamba ni wajibu wa kila kiongozi wa dini na wananchi kwa ujumla kuitunza vilivyo Amani ambayo imetupatia sifa ya kuwa kisiwa cha Amani katika Afrika.

Ndoa ya utulivu - Pepo ya Dunia

Kutoka uk. 1

jamaa wa kila mmoja" (Hotba ya Ijumaa, Novemba 10, 2006).

Dada zangu wapendwa, inasikitisha kubaini kuwa hali halisi ilivyo katika familia nyingi hivi sasa ni kinyume na dhana hii. Kwa bahati mbaya siku hizi mahusiano yanadhoofika, matatizo katika ndoa yanaongezeka na idadi ya talaka inapanda. Mwenendo huu mbaya unadhihirisha kuwa kuna jambo halijakaa sawa kuhusiana na misingi ya ndoa na mahusiano ya udugu.

Huzur (atba) aliendelea kusema kwamba; "Kwa bahati mbaya, malalamiko juu ya suala hili (suala la ndoa) yanaendelea kuongezeka. Wakati fulani shutuma nzito huwa zinatolewa dhidi ya wanawake, wakati fulani wanawake wanateswa vibaya na ndugu za mume. Kama ingekuwa sio kwa rehema za Allah na amri Yake; "Basi ukumbushe" (87:10) kungekuwa na mtafaruku mkubwa na kukata tamaa. Hata hivyo, kwa kufuata amri ya Mtume Mtukufu (saw) na Masihi Aliyeahidiwa (as), kipaumbele kinatolewa kwenye kunasihiana na kushauriana". (Hotuba ya Ijumaa, Novemba 10, 2006).

Ninakiri mada hii ni nyeti sana, lakini napenda kujadili masuala maalum ya udugu na mahusiano ya ndoa, ambayo iwapo yataangaliwa na kuboreshwa yanaweza kuleta utulivu katika familia na bila shaka yanaweza kuleta taswira ya pepo majumbani mwetu.

Hata hivyo kabla sijaanza, kwa unyenyekevu nawaomba wasikilizaji wangu kujenga uvumilivu wa kutosha na ujasiri ili kusikiliza matatizo haya na kwa moyo mkunjufu, tujaribu kujadiliana juu ya ufumbuzi uwezekanao kwa migogoro na matatizo haya.

Dada zangu wapendwa, kwanza tuzitazame sababu za matatizo haya. Kuna sababu nyingi ziletazo maswala haya katika mahusiano ya ndoa. Nimechagua nne kati ya sababu zinazojitokeza mara nyingi zaidi; nazo ni:-

1. Kukosekana kwa Taqwa
2. Uchaguzi mbovu wa wenza
3. Kutokufahamu wajibu na majukumu
4. Maingilio mabaya ya wazazi

Kukosekana Taqwa

Wakati fulani tunashuhudia kuwa pande zote (familia zote) zina upungufu katika Taqwa. Tabia zao na mitazamo yao katika maisha yao ya kila siku zinathibitisha wazi kabisa kwamba wameenda mbali na maamrisho ya Allah Mwenye Enzi na mafundisho ya Mtume Mtukufu (saw). Taqwa ndio mzizi wa kila tendo jema. Hadhrat Masihi Mauud (as) amesema; "Wako mbali na Mungu wale walio mbali na Taqwa"

Zaidi ya hapo, mpendwa wetu Mtume Mtukufu (saw) ametushauri kwamba; kusema kweli na kuambatana na 'Qawl-e-sadidah', kauli nyofu, yapaswa kuwa alama ya muumin wa kweli. Hili ni jambo ambalo siku zote litapelekea kupatikana kwa mahusiano yenye amani. Kinyume na hayo, hata hivyo, aghalabu huonekana mara nyingine watu huchagua kuficha ukweli, wakakosa ustahimilivu kwa mapungufu ya wenzao na wakawa si wasamehevu. Tabia kama hii huzusha khulka mbaya kama kiburi na kujiona. Kuhusu hili, Hazrat Khalifatul Masih V (atba) ametoa ushauri ufuatao, "subira na upole ni khulka njema ambazo tunapaswa kuzikuza kati yetu"

Tunapaswa daima kukumbuka mafundisho ya Qur'an Tukufu. Allah Mwenye enzi Amesema; "Hakika Aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi".

Kwa hiyo inakuwa hakuna budi kwa Waislam ila kufanya ukuzaji wa Taqwa, au ucha Mungu kuwa kipaumbele cha juu zaidi na lengo kuu la maisha yao. Kwa bahati mbaya, tunaona leo kwamba tamaa za kidunia na mambo yasiyo na maana yamechukua mahala pa lengo hili adhimu. Tunapotea kutoka katika "njia iliyonyooka". Hili kengeuko kutoka katika lengo letu linaleta kutoridhika, kukosekana utulivu na magomvi katika familia na udugu. Hivyo hii ndio sababu ya kwanza inayoweza kuleta kutoweka kwa amani niliyotaka kuijadili.

Uchaguzi wa wenza

Sababu ya pili ninayotaka kuijadili ni uchaguzi mbovu wa wenza. Nitapenda kuanza na usemi wa Mtume Mtukufu (saw), amesema: "Mlete mwanamke Mcha Mungu, (atakusaidia kutimiza majukumu yako)". Usemi huu wenye shani unamaanisha kwamba wakati wa kufunga ndoa, pande zote mbili zapaswa kupembua kwa makini na kuelewa wajibu wao kila mmoja na majukumu yao. Familia ya mume wasimfungishe ndoa kijana wao wakiwa na lengo la siri kwamba mke aje kuwatumikia. Kinyume chake, Mtume Mtukufu (saw) wa Islam daima amewaasa wanaume kuoa kwa nia na hamu kuwa mwanamke achaguliwe ambaye pamoja na kutimiza wajibu wake atamkumbusha pia mumewe naye kutimiza majukumu yake na kwa pamoja wanandoa watatimiza wajibu wao wote ambao wamefaradhishiwa na Allah. Kwa hakika migongano katika jamii tunayoishuhudia leo itapungua ikiwa ndoa zitafungwa kwa malengo kama haya.

Mwanaume hatakuwa na chuki kwa ndugu za mke na m ke hatawakosea adabu wanafamilia wa mumewe, na watasaidiana katika kutimiza wajibu wao. Huu ndio msingi ambao kwao amani inaweza kuletwa na bila shaka itazaliwa katika jamii mbali mbali duniani.

Ikiwa familia ya binti inayo lengo la siri kwamba mumewe awatumikie wao na sio wazazi wake, na ndugu za mvulana wanadai kwamba msichana asiwahudumie wazazi wake bali awatumikie wao, hapo jamii kama hii haitaweza kuufikia utulivu, na amani haitaweza kujengwa duniani.

Inasemwa, kichwa hakiwezi kuwa na amani wakati mkono unapouma, hali kadhalika mume hawezi kuwa na utulivu wakati mkewe anahuzunika na mke hawezi kuwa na furaha wakati mumewe anataabika. Ndugu wa mume na wa mke hawatafarijika wakiwaona vijana wao hawana furaha. Ikiwa tutaifahamu hekima ya msemo huu na tukazingatia vyema hali ya majukumu tuliyonayo baina yetu, bila shaka tutaishi kwa amani". (Khutbat-e-Mahmud).

Nilisema mwanzo kwamba sababu ya tatu ni kukosekana elimu na uelewa barabara juu ya wajibu na majukumu baina ya wanafamilia kwa kuzingatia mawaidha haya ya Hadhrat Muslih Mauud (ra), nitageukia sasa baadhi ya majukumu ya waume, wake na wazazi wao katika kujenga nyumba yenye utulivu.

WAJIBU WA MUME

Katika Qur'an Tukufu, Allah Anasema; "Wanaume ni walinzi wa wanawake kwa sababu Mwenyezi Mungu Amewafadhili baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya mali zao wanazozitoa, basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanaohifadhi (hata) wasipokuwapo (waume zao) yale Aliyoyahifadhi Mwenyezi Mungu".

Moja ya majukumu ya mume Mwislam ni kutimiza wajibu wake wa 'Qawwam' (Mtunzaji na mlinzi). Mwanaume ambaye anajifananisha kiukweli na 'Qawwam' yaani anao mwenendo adhimu ana mtazamo wa huruma, ni mstahimilivu, huyasamehe makosa madogo madogo, anayamudu maisha yake ya ndoa, ni mkarimu bila kuwa mharibifu wa mali.

Anaheshimu maoni ya mke wake na anamfanya ajisikie mshiriki katika jukumu la kuendesha masuala ya nyumba, kutunza watoto, na kushirikiana na mumewe katika kujenga familia imara ya kiislam, kama itakiwavyo na Islam.

Kuna usemi maarufu wa kiongozi wetu mpendwa, Mtume Mtukufu (saw) aliosema; "Mbora wenu ni yule aitendeae familia yake wema zaidi, nami ni mbora wenu katika kuitendea wema familia yangu" (Mishkaat).

Zaidi ya hapo Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema; "Ninamuona mtu anayepigana na mkewe kuwa ni mwoga na hana uanaume kabisa" (Malfuzat, vol.2 pg.387). Masihi (as) pia alisema ; "Mtu asiyekuwa na huruma na wema kwa mke wake na ndugu za mke wake hayumo katika jamaa yangu". Kila mume ambaye si mwaminifu kwa mke wake na kila mke ambaye si mwaminifu kwa mumewe hayumo katika jamaa yangu". (Safina ya Nuhu, Ruhani khazain, vol.19,pg.19).

Kuhusiana na mada hii, Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) amesema katika moja ya hotuba zake kuwa; "Allah Amemuumba mwanaume na nguvu zaidi kuliko mwanamke ili aweze kubeba majukumu zaidi kama mkuu wa familia, kama mume na kama baba. Ili kuwa mfano mwema, mume ni lazima awe katika daraja la juu la Taqwa kiasi familia katika nyumba yaweza kufuata mfano wake katika maisha, ili kufikia daraja hili la Taqwa maombi maalum yanahitajika ya mtu mwenyewe na ya familia pamoja na jitihada binafsi" (Hotuba ya Ijumaa, July 2, 2004).

Huzur (atba) akafafanua kwamba Mtume Mtukufu (saw)nimfanoborakabisakwetu kufuata katika kustawisha familia yenye siha na imara. Akinukuu hadithi mbalimbali Huzur (atba) alijadili mfano wa Mtume Mtukufu (saw) kuwa ndio mume bora kabisa na mkuu bora kabisa wa familia.

"Akiwa ni mkuu wa familia mume anawajibika kukidhi mahitaji ya mke wake na watoto. Anapaswa kutumia muda na familia yake, kuwaleta katika matukio ya Jamaat na kuwa sehemu ya matakwa yao na matatizo yao. Katika maisha ya kila siku, tunaona kwamba kiongozi mwenye mafanikio ni yule ambaye anayaelewa barabara matatizo yaliyomo kwenye duara la wa wajibu wake".

"Hebu na tuitazame hali ilivyo majumbani hivi sasa. Baadhi ya wanaume huwatendea wake zao vya kusikitisha, hawawaheshimu na hawazijali hisia zao. Wengine wana viganja vilivyokunjika mno na hutumia mikono yao juu ya wake zao. Nje ya nyumba zao huonyesha picha ya ucha Mungu mpevu, huruma na ukarimu, lakini ikija katika mishabaha na wake zao na watoto wao, wanapinduka kuwa watukanaji na wachoyo"

Hadhrat Khalifatul Masih V

Endelea uk. 4

Uhai wa Islam unapatikana wapi?

Kutoka uk. 1

amefanywa kuwa Mujaddid. Masihi aliyeahidiwa (as) anasema, "Mungu Amenituma kuirejesha imani ambayo ilitoweka katika ulimwengu huu na kuwahuisha wanadamu, baada ya kupewa nguvu kutoka kwa Mungu, na kuwavuta watu kuelekea kwenye wema na kuwaokoa katika uovu. Nimekuja pia kuonesha kwamba, kinyume na Qur'ani Tukufu vitabu vingine vyote vya dini havina athari yoyote.

Huzur (atba) akasema kwamba njia zote zilizopatikana sasa kwa ajili ya kueneza Islam katika zama hizi ni ishara pia kwa ajili ya Masihi aliyeahidiwa (as).

Allah Alimpatia Masihi aliyeahidiwa (as) habari njema kwamba baada yake ujumbe wake utaendelezwa na taasisi ya Khilafat. Leo tunashuhudia kutimia kwa bishara hii na kazi ya kubashiri Islam inaendelea duniani kote chini ya usimamizi wa Ukhalifa. Sawa na bishara, Ukhalifa huu utaendelea mpaka kiyama. Hii inaonyesha kwamba Mujaddidin watakuwa si wengine bali Makhalifa ambao wanaendeleza kazi ya Masihi aliyeahidiwa (as). Kwa baraka za Ukhalifa kazi ya uhuishaji inaendelea duniani kote sio tu kupitia Wabashiri bali hata Waahmadiyya wa kawaida.

Huzur (atba) akasema, hata leo Allah Anaonyesha ishara kubwa kubwa kuusaidia Ukhalifa na Anawaongoza watu kwa Masihi aliyeahidiwa (as). Allah Anawaonesha Makhalifa kwenye ndoto za watu wema kama ishara kwamba Ukhalifa ndio njia ambayo kwayo kazi ya kueneza Uislam inafanyika.

Huzur (atba) akasema kila Ahmadiyya anapaswa kuwa na imani thabiti katika madai yote ya Masihi aliyeahidiwa (as) na kuendeleza ujumbe wake kwa kufanya mabadiliko mema ndani yake mwenyewe na kwa familia yake. Tuacheni bidaa potovu na tuweni wasaidizi wa Masihi aliyeahidiwa (as). Allah na Atuwezeshe kutimiza hayo. Amin.

Ndoa ya utulivu - Pepo ya Dunia

Kutoka uk. 3

(atba) akaendelea kusema; "Wakati mwingine katika magomvi ya familia, wazazi wanakimbilia kuchukua hatua za mwisho na kumwamuru mume kumfukuza mke kutoka nyumbani na baadhi ya waume wanaitikia na kutekeleza ukatili huu. Wanaume kama hawa hawastahili kuitwa "Wanaume". Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema; "Mume na mke wanapaswa kuishi pamoja kama marafiki wazuri sana. Wale wasiowatendea wema ndugu za wake zao hawamo katika Jamaat yangu".

Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema pia; "Uhusiano mume anaokuwa nao na mkewe unapaswa kuwa kama ule baina ya marafiki wawili wa kweli. Wake ndio wa kwanza kushuhudia khulka zake njema na uhusiano wake na Allah. Kama uhusiano wake na mkewe sio mzuri, basi atawezaje kujipatanisha na Mungu". (Malfuzat, vol.3 pg.300).

Hivyo hizi zilikuwa baadhi ya sifa za mume mwema ambazo ni za lazima katika kuleta ndoa yenye mafanikio.

SIFA ZA MWANAMKE MWISLAM

Sasa nitaangazia baadhi ya majukumu na sifa za mke mwema. Kisha twaweza kutafakari kama tunakidhi viwango hivi.

Kwanza kabisa mke anapaswa kuyaheshimu matakwa ya mume wake kwa kumtii yeye katika mambo yote mazuri na ya wema. Kadri anavyoyajali mashauri yake, matakwa na maelekezo ndivyo wanavyozidi kuwa na furaha na faraja zaidi katika ndoa yao na hii ni karibu zaidi na mafundisho na dhati ya Islam. Mke Mwislam, utii wake kwa mume wake imesemwa, waweza kwa hakika kumuwezesha kuingia peponi. Kama alivyosema Mtume Mtukufu Muhammad (saw); "Mwanamke anayesali sala tano, anayefunga Ramadhani, ni mtiifu kwa mume wake na huyakubali maelekezo yake ataruhusiwa kuiingia pepo kwa mlango wowote atakaopenda"! (Tibrani).

Tena sifa ya mke mwema ni kwamba humheshimu mumewe na daima anakuwa na hamu ya kumpendeza na kumfurahisha. Kama mumewe yu maskini, halalamiki juu ya upungufu wa matumizi. Halalamiki juu ya kazi zake za nyumbani, kwa kuwa anakumbuka kwamba wake wengi wema katika historia ya Islam wameonyesha mfano wa subira, hisani na mtazamo chanya katika kuwahudumia waume zao na kutunza nyumba zao bila kujali umasikini na taabu walizozikabili.

Alitokea mwanamke aliyemjia Mtume Mtukufu (saw) ili kumuuliza suala fulani, na alipokwisha kulishughulikia. Alimuuliza (saw) "Je unayemume?" akasema, "ndiyo". Akamuuliza (saw), "Unaendeleaje naye?" Akajibu, "Siachi kutimiza majukumu yangu, ila kwa yale yaliyo nje ya uwezo wangu". Akamwambia (saw), "Uwe mwangalifu katika jinsi unavyomtendea, kwa kuwa yeye ndio pepo yako na jahannam yako". (Ahmad, Al-Albani & others. Al-Tarhlib wal -Tarhib, 3/52, kitab Al-Nikah).

Kwa kuzingatia ushauri wa Mtume Mtukufu (saw), twaweza kuchagua njia ya kwenda peponi au motoni sisi wenyewe. Wapo wanawake ambao hawawaheshimu waume zao, au hawawapi hadhi wanayostahili, kwa hiyo nitapenda kila mmoja kujitazama mwenyewe na kuona kama tabia zetu wenyewe na vitendo vinaendana na daraja tunaloelekezwa kwa busara ya mafundisho ya Mtume Mtukufu (saw).

Mtume Mtukufu (saw) aliwahi kusema, "Mbora kati ya wanawake ni yule aletaye furaha kwa mume wake kila anapomtazama. Anamtii kila anapomwelekeza kufanya jambo fulani na ni mwangalifu kuhusiana na mali yake na utu wake, na anaepuka matendo yote yale yawezayo kumkera mume wake". (Mishkaat).

Zaidi ya hapo, Masih Aliyeahidiwa (as) amesema, "Kipande kikubwa cha heshima ya waume zenu kipo mikononi mwenu. Timizeni wajibu wenu kwa waume zenu kwa bidii ya moyo ili mhesabiwe katika wema na watii mbele ya Mungu" (Kashti Nuh, ruhani khazain vol. 19, pg.81).

Nitapenda pia kunukuu mawaidha ya Hadhrat Nawab Mubarak Begum sahiba (ra); "Baada ya ndoa, kwanza mke anakuwa mtumwa kwa mumewe kisha mume anakuwa mtumishi kwa mkewe". Usemi huu umejaa hekima kubwa, kwanza mke anakuwa mtiifu na kumfuata mumewe na hivyo anaushinda moyo wa mumewe na mume humpenda".

Anaendelea kusema; "Msibainishe mambo ya siri baina ya mume na mke kwa watu wengine. Wake huwaeleza rafiki zao na waume huwaeleza rafiki zao mambo fulani na kujitapa kwa namna ambayo si yenye kufaa wala si ya welekevu".

Sifa nyingine ya mke mwema ni kwamba anamtendea mama mkwe wake na familia ya mume wake kwa wema na heshma. Njia mojawapo ya mke kuonyesha heshima kwa mumewe ni kwa kumjali na kumheshimu mama ya mumewe. Anajua kwamba mtu aliye na haki zaidi kwa mwanaume ni mama yake. Hakuna kitakachomfurahisha mwanaume anayejiheshimu, mwema na anayejali kama kuona uhusiano imara wa mapenzi na heshima kati ya mkewe na familia yake.

Ili kulinda amani katika ndoa, mke anapaswa kuielewa saikolojia na maumbile ya mume wake na anapaswa kutambua lipi humfurahisha na lipi humkasirisha. Anapaswa kuwa na uwezo wa kuutwaa moyo wa mume wake na kustahili kusifiwa na heshima kutoka kwa mume wake, na anapaswa kufunga mlango kwa lolote linaloweza kuleta ugomvi unaoweza kuharibu maisha ya ndoa.

Sasa nitapenda kuzitaja baadhi ya Hadithi ambamo Mtume Mtukufu (saw) ametuonesha mke mwema anatakiwa awe vipi; "Ikiwa mwanamke anafariki na mumewe yuko radhi nae, basi ataingia peponi" (Mishkat).

Mwanamke msifika humsaidia mumewe kumcha Mungu kwa namna mbalimbali, hususan katika kuamka na kusali usiku.

Kuhusiana na hili Mtume Mtukufu (saw) amesema; "Allah na ambariki mwanaume ambaye huamka usiku kwa sala na humuamsha mke wake asali, na asipoamka humdondoshea matone ya maji usoni mwake. Na Allah ambarikie mwanamke yule ambaye huamka usiku kwa sala, na humwamsha mumewe na asipoamka humdondoshea matone ya maji usoni kwake".

Sifa nyingine ya kupendeza ya mke mwema ni kwamba hazielezi siri za mume wake na mambo mengine binafsi yanayoweza kuwa kati ya mume na mke. Hadhrat Nawab Mubaraka Begum (ra) sahiba kwa msisitizo anawashauri wanawake kuwa, "Msifanye jambo lolote kwa siri, mkijisikia jambo fulani imebidi mlifanye sirini, basi msilifanye jambo hilo kabisa. Ikiwa mume wako atagundua basi utapoteza imani yake kwako moja kwa moja, na hii itakuwa ni pamoja na fedheha na aibu utakayojisikia".

Mafundisho ya Qur'an Tukufu kuhusu hili ni kama haya; "Wao ni nguo kwenu, nanyi ni nguo kwao" (2:188). Hadhrat Khalifatul Masih I (ra) alipata kusema; "Kama ambavyo nguo hutoa faraja, raha na ulinzi dhidi ya joto, hupendezesha na hulinda dhidi ya maumivu mbalimbali, hali ni kama hiyo hiyo kwa wanandoa. Kama ambavyo nguo hufunika mapungufu, hali kadhalika waume na wake hufunika mapungufu ya kila mmoja wao" (Khutbat Nur, pg.400).

Kwa hivyo dada zangu wapendwa hizi ndizo sifa za mke mwema. Kama mke atashika sifa hizi basi huenda akapata sio tu ridhaa ya mume wake, bali baraka za kimbingu pia. "Nyumba ni mahala panapoangazwa na mishumaa ya mapenzi na maaminiano. Ni mahala palipojengwa kwa mapenzi kwa fadhili za Allah. Nyumba ni mahala ambapo huondoa uchovu wa mtu baada ya kazi za siku nzima. Nyumba huendelezwa kwa mapenzi. Ni mwanamke ndiye aifanye bustani hii yenye faraja. Nyumba si nyumba bila mwanamke"

Wakati mwingine wanawake hawazingatii mambo haya na huwa ni sababu ya magomvi kwao wenyewe. Kwa mfano, wakati mwingine wanawake hushauriana wao kwa wao kwamba ikiwa utammiliki mume wako tangu siku ya kwanza ya ndoa, au mwanzoni mwa maisha yako ya ndoa, basi utaweza siku zote kumtawala.

Dada zangu wapendwa, jambo hili ni upotovu mno na kimaadili ni ushauri mbaya. Ikiwa mwanamke atajiingiza katika jitihada hii isiyo na maana, bila ya shaka hataweza kuheshimiwa na mume wake, na kamwe hataweza kujenga pepo yake ya duniani.

Siku hizi jambo jingine limejitokeza ambalo husababisha maanguko ya haraka katika afya zetu za kimaadili na kiroho, na hivyo kuanzisha mizozo baina ya jamaa nalo ni matumizi ya simu yaliyozidi kiasi. Siku hizi simu za kitaifa ni bure na baadhi ya wanawake hutumia muda mrefu kuongea, kupiga soga na kuwasengenya wengine. Sio tu kwamba hii ni upotezaji mkubwa wa wakati, bali kwa kujiingiza katika masengenyo tunayajaza matumbo yetu kwa moto wa jahannam, kwa maana kuna usemi wa Mtume Mtukufu (saw) usemao kwamba; "Yule anayesengenya kamwe hatoingia peponi".

Kuhusiana na hili Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) amesema, "Ndoa baina ya mume na mke inachukua sura ya mkataba. Mwanamke ameamriwa kwamba anayo majukumu kama vile kuangalia mahitaji ya mume wake, kutunza watoto, kuangalia masuala ya nyumba n.k. Vivyo hivyo, mwanaume nae anayo majukumu kama kuangalia matumizi ya familia, na mahitaji mengine n.k. Kwa hiyo kadri mume na mke wanavyotimiza mkataba huu, ndivyo jamii nzuri zaidi itakavyojengwa. (Hotuba ya Ijumaa December, 19, 2003).

Kwa bahati mbaya, wakati mwingine matatizo hutokea kwa sababu ya mtu mmoja kuzembea katika kutimiza majukumu yake. Kwa mfano, wakati mwingine tumeona kwamba baada ya ndoa, mwanamke anaendelea kumtembelea au kuongea na mama yake au ndugu zake wengine, kwa kiwango cha kupita kiasi au kisichopendeza.

Haya mawasiliano ya mara kwa mara huchujisha nguvu ya maaminiano kati ya mume na mke kwa kuwa habari za ndani ya nyumba zitokazo kila siku nyumbani zinasambazwa kwa jamaa wengi. Hata kwa nia njema kabisa, hawa watu wa nje wanaweza moja kwa moja au kwa namna nyingine kuhusika katika kuleta mizozo na machafuko kati ya wanandoa kwa ushauri wao na nasaha zao.

Kwa hiyo, mke mwenye busara anapaswa kuepuka tabia kama hii isiyopendeza, hasa kwa vile inao uwezekano wa kuja kuwa chanzo kikubwa cha magomvi nyumbani mwake.
Vilevile mamboyanayoonekana madogo huwa yanapelekea kutokea kwa maumivu mazito katika mahusiano, kwa mfano, pale mke anapozira au kukaa kimya kisicho kawaida kwa muda mrefu hali kadhalika kama hamkaribishi mumewe kwa moyo mkunjufu pale mume anaporejea nyumbani au anamkatisha mumewe katika mazungumzo au kutumia maneno mbele ya watu ambayo yanamkosea heshima mume wake au kujiingiza katika malalamo ya hasira.

Vilevile mume akimwomba wale chakula pamoja husema; "Hapana, sina njaa". Mume akipendekeza dawa kwa ajili yake husema, "hapana, sitaitumia kwa kuwa haitanisaidia". Mume akileta zawadi yoyote, anaitazama kwa bezo. Haya yanaonekana ni mambo madogo madogo katika tabia zetu, lakini kama hayakutambuliwa na kurekebishwa mapema, yanaenda mbali na kuzalisha machungu katika maisha ya wanandoa.

WAJIBU WA MAMA MKWE

Mwisho, nitapenda kujadili wajibu wa akina mama mkwe. Kwa bahati mbaya wanaweza kuwa chanzo cha misuguano na mizozo katika familia. Hata hivyo, wakati mwingine akina mama wakwe wanatendewa vibaya na wake za watoto wao. Baadhi ya wanawake wanashindwa kuwapatia heshima na haki ambazo ni stahiki kwa mama za waume zao. Kwa upande mwingine baadhi ya akina mama hawawapi nafasi watoto wao kutimiza wajibu wao kama waume wazuri. Akina mama kama hawa hutumia hadhi yao

Endelea uk. 5

Kutoka uk. 4

ya kuwa wazazi, na kujiona wanayo haki peke yao ya kuangaliwa na watoto wao wa kiume.

Kuna hadithi inayosema; "Hakuna awezaye kuwa Mwislam mpaka ampendelee pia nduguye kile akipendacho yeye mwenyewe". Falsafa hii hii ndiyo ipasayo kutumika katika hali hii. Mama mkwe ni lazima amheshimu mkwewe na ampe nafasi ya uhuru pale nyumbani, kwa namna ile ile alivyohitaji kwa ajili yake alipokuwa mkwe mpya na atakavyopenda iwe kwa mabinti zake mwenyewe katika ndoa zao. Inaonekana mara kwa mara kwamba akina mama wanakuwa na mapenzi pale wanaposhughulika na mabinti zao wenyewe lakini kwa ajili ya wakwe zao, wanaonesha mwenendo mwingine.

Hadhrat Khalifatul Masih V(atba), akisisitiza juu ya kusimamisha Taqwa anaiasa Jamaat kuchunga na kuwa na mtazamo wa busara katika mambo ya mahusiano ya kindoa, na zaidi katika masuala nyeti baina ya akina mama mkwe, wake na mawifi.

Huzur (atba) aliziombea nyumba za Waahmadiyya kwamba washikamane na Taqwa katika mambo yahusuyo

Ndoa ya utulivu - Pepo ya Dunia

mahusiano ya kifamilia katika ndoa. (Hotuba ya Ijumaa, May 30, 2003).

Katika tukio jingine Hadhrat Khalifatul Masih (atba) amesema; "Siku hizi, baadhi ya watu hawawaangalii na kuwajali wake zao kwa sababu tu watu fulani watasema kwamba mume fulani anakuwa mtumwa kwa mke wake. Kwa kweli kinachoshangaza ni kuwa hata baadhi ya wazee wa familia ya mume humwambia asiwe mtumwa wa mke wake, badala ya kuhimiza upendo na kuheshimiana kati ya mume na mke. Watu kama hawa wanatamani kitu kimoja kwa ajili yao wenyewe na kitu tofauti kwa wenzao". (Hotuba ya ijumaa July2, 2004, Khutbat Masroor, vol.2 pg.454).

Ili kuweza kufafanua zaidi na kuelezea somo hili nyeti, nitapenda kuainisha baadhi ya mambo ambayo yakifanywa na mama mkwe na mkwe yatachangia kuleta utengamano katika nyumba.

MAMBO YA KUFANYWA NA MAMA MKWE

- Mpende mkwe wako kama binti yako mwenyewe
- Heshimu matakwa, tamaa na matarajio ya mkwe wako. Muunge mkono katika kila jambo jema.
- Ikiwa mkwe wako ametenda kosa zito tafakari kwanza hali ilivyo kabla ya kumsahihisha.

Kumbuka watoto wako vilevile hufanya makosa kwa hiyo mtendee nae kwa mapenzi kama wao.

- Jiambue na uwape nafasi watoto wako waliooana wayaendeshe maisha yao ya ukubwani, kwa ujumla, USIINGILIE katika maisha yao ya kila siku.

MAMBO YA KUFANYWA NA MKE

- Ingiza ndani yako badiliko la moyo wakati wa "Rukhsati". Ni muhimu kwamba kwa wewe kupita njia hii ambayo hujapata kuipata ukiwa na mume wako na familia yake kuelekea kwenye nyumba mpya na ambayo ndiyo nyumba yako ya kweli, yapaswa ujenge mapenzi ya kweli kwa mume wako na uyapende pia yale ambayo ni muhimu kwake. Haya ni pamoja
na familia yake.

- Bila shaka ni kawaida ya kimaumbile kuwa unawapenda wazazi wako, kaka zako na dada zako ambao umekuwa pamoja nao kwa miaka ishirini, thelathini au zaidi. Nawe Allah
Akikupa miaka 90 ya kuishi basi huenda utakuwa unaishi na mume wako kwa miaka 70 ijayo.

- Unapowasili katika nyumba yako mpya, kila kitu kitakuwa kipya na tofauti na waweza kujikuta unajisikia ugumu fulani. Hii yaweza kukufanya urejee ulikotoka, kwa familia yako, kwenye mazingira uliyoyazoea. Wapaswa kulikwepa wazo hili na kuepuka tamaa ya kurudi nyumbani mapema mno. Jipe muda na nafasi ya kuitambua familia yako mpya na kuizoea nyumba yako mpya.

- Mara unapoolewa na kuondoka katika nyumba ya wazazi wako, wazazi wako inaeleweka watajisikia huzuni na watatamani sana uwe pamoja nao. Wanaweza kutaka kufahamu kila kitu katika maisha yako ya ndoa, na wanaweza kukuomba uwatembelee mara kwa mara.

Bila shaka kuna shinikizo la kutowaangusha wazazi wako. Kwa vyovyote wapaswa kuwatembelea wazazi lakini sio kwa kupoteza muda wa thamani unaouhitaji katika kujenga uhusiano na mume wako na familia yake. Ni kwa faida yako ya baadae kujipatia imani na
heshima kutoka kwa familia ya mumeo.

- Kutakuwa na wakati ambapo utapenda kuwaambia wazazi, kaka na dada zako yale yote yanayosisimua katika maisha yako. Kuwa muangalifu na kuepuka kuanika kila kitu
kinachotokea katika nyumba yako mpya.
- Kipaumbele chako kiwe ni kujenga maisha yako mapya. Inafanana na kupanda mbegu, kumwagilia, kuzipalilia na kuziona zikukua na kusubiri maua na matunda.

- Pale inapowezekana, jaribu kutomwonesha manung'uniko, malalamiko au hadithi ndefu za
masikitiko kwa mume wako mara arudipo nyumbani.
- Uwe na uangalifu maalum kwa usafi na afya ya nyumba. Vaa nguo za kawaida lakini zinazovutia ukiwa nyumbani na weka nywele, kucha na meno yako katika hali ya usafi na unadhifu.

Daima uuamini msemo huu; "Ikiwa ninaamini, naweza kufanikisha!". Mahusiano kati ya mama mkwe na mkwewe ni ya thamani. Yanaweza kuwa sababu ya nguvu kubwa na umoja katika familia. Wote hawanabudi kujenga uhusiano huu, wote wanapaswa kuwa tayari kujitolea na wanapaswa kumtendea kila mmoja kama wanavyotaka wao kutendewa.

Masihi Aliyeahidiwa (as) amesema; "Binti anapoolewa anakuwa na funguo mbili mikononi mwake, mmoja ni wa mlango wa amani na mwingine ni wa mlango wa magomvi. Aweza kufungua mlango wowote aupendao. Wamebahatika wanawake wale wanaofungua mlango wa amani. Mwanamke ni lazima ajithibitishe kuwa ni mtiifu. Wanawake ambao, wanawashauri wanaume zao kutokuwa watiifu kwa wazazi wao wana bahati mbaya mno. Hawataweza kamwe kupata furaha ya pamoja". (Sirat Hadhrat Nawab Mubaraka Begum sahiba, pg.343).

HITIMISHO

Nyumba hujengwa kwa mapendo. Dada zangu wapendwa ni ukweli usiopingika kwa mifano ya kweli ya nyumba za Kiislam ambazo zinawakilisha amani, kuridhika, maelewano na utulivu kwa hakika zimejengwa kwenye msingi imara wa upendo, heshima na kujitoa. Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) amesema; "Nyumba ni mahala panapoangazwa na mishumaa ya mapenzi na maaminiano. Ni mahala palipojengwa kwa mapenzi kwa fadhili za Allah. Nyumba ni mahala ambapo huondoa uchovu wa mtu baada ya kazi za siku nzima. Nyumba huendelezwa kwa mapenzi. Ni mwanamke ndiye aifanye bustani hii yenye faraja. Nyumba si nyumba bila mwanamke". Hotuba ya ijumaa, June 24, 2005)

Katika Islam ndoa ni mkataba uliobarikiwa kati ya mwanaume na mwanamke, na wanaianza safari ndefu ya maisha kwa roho ya upendo, ushirikiano, mtangamano na kuvumiliana, ambapo kila mmoja hujisikia raha akiwa na mwenziwe na hupata utulivu, kutosheka na kuliwazwa awapo pamoja na mwenzake.

Qur'an Tukufu imeeleza uhusiano huu baina ya wanaume na wanawake ambao huleta mapenzi, utulivu, kuaminiana na kuhurumiana katika lugha inayovutia na fasaha mno. "Na katika ishara zake ni kuwa Amewaumbieni katika jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao, Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu" (30:22).

Hadhrat Khalifatul Masih v (atba) amesema pia; "Machungu yaliyopo katika jamii zetu leo yanaweza kuondoshwa. Leo na tufanye ahadi kwamba tutajenga mifano mizuri ya ucha Mungu, tutasamehe makosa ya wake zetu na waume zetu. Ndipo kwa njia hii mahangaiko yaliyozalika katika familia mbali mbali kwa sababu ya mitafaruku itaweza kuondoshwa". Huzur (atba) akasema kwamba "Wale waliokuwa wamegubikwa na mitafaruku ya ndoa hata kama wamefikia hatua ya kuachana, watumie hali ya kiroho iliyopo katika Jalsa, kufanya maombi, kujaribu kuunganisha nyoyo zilizovunjika, kusamehe, kutowalaani wengine, kusitiri makosa ya wenzao na kukumbuka makosa yake mtu mwenyewe na daima kutazama namna Allah Anavyosetiri madhambi yetu yasiyohesabika. (Hotuba ya ijumaa, June 24, 2005).

Zaidi ya hapo, Hadhrat Khalifatul Masih IV (rh) alipata kusema; "Sala na kumkumbuka Allah huzigeuza nyumba kuwa pepo, sifa hizi mbili zilivyo ni kwamba husababisha wote (waume na wake) kupata msaada kwa hivyo elekezeni mawazo yenu katika kumkumbuka Allah. Ndimi zenu na nyoyo zenu ziwekeni mashughuli katika salat, kumkumbuka Allah na Durud sharif". (Hotuba ya ijumaa, August 5, 1983).

Nitamaliza hotuba yangu kwa maombi haya ya kupendeza; "Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na utujaalie kuwa viongozi wa wamchao Mungu" (25:75).

Allah na Atuwezeshe kujenga utulivu katika nyumba zetu na kuzifanya nyumba zetu kuwa ni taswira ya pepo duniani.
Amin.

Makala hii imefasiriwa kutoka Kiingereza na Bw. Mussa Awadhi Mpinga.

Bukkede Afrika

Na Mahmood Hamsin Mubiru, Dar es Salaam

Wakati tumetimiza nusu karne ya uhuru wa Tanzania bara, kiongozi wa Jumuiyya ya Ahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alimtumia salamu za pongezi Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa taifa lake kutimiza umri huo wa uhuru.

Ujumbe wake ulikuwa mzito na katika mengi yaliyosemwa katika ujumbe huo, tutatizama kwa hivi leo ombi la kiongozi huyo wa kiroho aliyewataka viongozi wa Afrika wawe watumishi wa watu na wasifuje mali za watu wao.

Afrika imekuwa na bahati mbaya ya kuwa na viongozi wafujaji wa mali za uma waliofurutuada. Wapo wengi viongozi wa sampuli hiyo ila katika makala haya tutamtizama Mheshimiwa, Mtukufu Rais Mfalme wa maisha Jean Badel Bokassa wa Jamhuri ya Afrika ya kati.

Mwanaume huyu wa shoka Jean Badel Bokassa alizaliwa mwaka 1921. Alijiunga na jeshi la Ufaransa na kuwa askari muaminifu. Uaminifu huo ulimpeleka hadi Vietnam ambako alipigana bega kwa bega na Wafaransa dhidi ya Wa Vietnam. Mapenzi yake kwa Wafaransa yalikuwa siyo ya kawaida. Yalikuwa mazito kiasi hiki ya kwamba alipofariki aliyekuwa Rais wa Ufaransa Charles de Gaulle, muheshimiwa huyo alilia kadamnasi na kupayuka "Papaa amefariki".

Mwaka1965alimpinduashemeji yake na kuanza utawala ambao umeweka doa katika historia ya Afrika. Desemba 1977 Mfalme Bokassa aliapishwa kuwa Mfalme wa nchi hiyo bila ya kujali hali ya umasikini wa watu wake. Taji alilovaa siku hiyo lilinunuliwa kwa bei ya paundi milioni tatu na sherehe nzima za yeye kuapishwa kuwa Mfalme zilighariimu paundi milioni nane. Bokassa alitumia fedha zinazofikia zile nchi inazozipata kama msaada kutoka Ufaransa. Msaada wenye uwezo wa kuiendesha nchi kwa miezi kumi na mbili matumizi mabaya yalioje? Khalifa wa Mwenyezi Mungu anapotoa onyo hilo kwa viongozi wa Afrika ni kwamba ana takwimu sahihi.

Wakatisherehehizozinaendelea wananchi wa Jamhuri ya Afrika ya kati walikuwa utumwani katika migodi ya dhahabu na mashamba ya kahawa ambapo kila mmoja alipata paundi 16.50 kwa mwaka . Jaribu kufanya

Endelea uk. 7

Bustani ya Washairi

ATI KWELI MALI HII - YAKALIWA NA SHETANI?

1 Ninaitafuta mali, kwa uvumba na ubani
Ile ambayo halali, hainayo dhambi ndani
Bali hakuna dalili, kuitia mkononi
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

2 Mali ninayoisema, ile vito ya thamani
Naisimamia wima, kuitafuta kwa shani
Walakini ninakwama, sijuwi sababu gani
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

3 Mara nyingi hajaribu, kuchimbuwa ardhini
Kuitafuta dhahabu, alimasi na madini
Ili nami nihesabu, bali mwisho siioni
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

4 Hazama kwenye makulu, makulu ya baharini
Kuitokonyowa lulu, lulu haipatikani
Nimeteza na mandilu, siyapati yapo chini
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

5 Nimeifata yakuti, huko huko baharini
Imekuwa hati hati, mifano kama utani
Mpaka huu wakati, hiyo yakuti sioni
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

6 Hata ile zumaridi, ngumu haionekani
Nimeifanya juhudi, ya dunia na ya dini
sijafikia kusudi, kupata vito jamani
Yakaliwa na shetani, ati kweli mali hii?

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
Dar es salaam.

HONGERA

1 Wana Katoma hongera, Jamaati imewini
Mmejenga jengo bora, nyumba yake Rahmani
Msikiti unang'ara, ushindile wa zamani

Mola Awape thawabu, akhera na duniani

2 Mlizisoma alama, jengo lile la zamani
Majira yameandama, muda myaka thalathini
Ndipo ikawa lazima, jengo jipya mjengeni
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

3 Inaihama baladi, Katoma si kijijini
Inaongeza idadi, kwenda kata za mjini
A'saa watafaidi, Msikiti wa thamani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

4 Heko raisi muhibu, abdul na Hamdani
Khalidi Issa katibu, michango yenu thamani
Mipango mliratibu, muamshe waumini
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

5 Khudamu kwa kila hali, mlivyo jitoleeni
Mumeikubali hali, kushinda msikitini
Ombi liwe maqbuli, nyote nawaombeeni
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

6 Lajna nisisahau, mchango wenu thamani
Ninyi ni washikadau, asubuhi na jioni
Yule wa kuwadharau, hatoingia peponi
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

7 Omari Bishazo heko, kujenga msikitini
Kwako liwe farijileo, mafao ya uzeeni
Dunia mahangaiko, akhera ni burudani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

8 Jengo zuri burudiko, thamani thumma thamani
Ona wake muezeko, umeboresha ramani
Maji kwa mtiririko, huingia kisimani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

9 Nondo za mviringiko, waya meshi dirishani
Rangi ni nzuri kuliko, imepakwa ukutani
Ukaweka matandiko, mazulia ya Irani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

10 Lingine kwenu chereko, Nyamihasi kumwamini
Aupeleke mwaliko, Kagenyi Jamaatini
Aje afanye mwandiko, Ahmedi Ramadhani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

11 Masjidl -Fat-hu, ufaulu wa imani
La ilaaha illallahu, kalima nambari wani
Muhammadur Rasulullah, wadaraja la thamani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

12 Inapendeza nakishi, nakishi msikitini
Mola Awape bakshishi, malipo kwa waumini
Mmekomesha ubishi, hapo Bukoba mjini
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

13 Mumekomesha ubishi, wameshindwa wapinzani
Walioleta uzushi, kutwita makadiani
Yakwao hayatutishi, maneno ya mitaani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

14 Walidai hatujui, maana za Kuruani
Wakuza yao laghai, waghiribu waumini
Sasa walete madai, twenende mashindanoni
Tuwafundishe kitabu, jinsi ya kuhami dini

15 Wapambe wale wabishi, wameachwa taabani
Wadai hatupwekeshi, Mola wetu Mannani
Kumbe ni wao utashi, kalima hawazioni?
Mola Wape matibabu, zing'arike zao mboni

16 Na Mtume Muhammad, wadai hatumwamini
Walinadi kwa juhudi, hadharani bila soni
Chuki yao Ahmadi, Masihi wetu zamani
Mbona wakosa adabu, kwa Mtume wa Manani

17 Roho yangu huburudi, kila nijapo nyumbani
Madereva nawanadi, nishushe msikitini
Lengo wanute uradi, wasome kalimatani
Mola Awape thawabu, akhera na duniani

18 Hayo ndiyo mahubiri, mbinu na mzibaini
Simba aliye hodari, hufaulu mawindoni
Lazima awe jasiri kuwinda nyati mwituni
Nahuo ndio wajibu, tukaishindishe dini

19 Mola Uwape thawabu, wale wanokuthamini
Idadi yao hesabu, kote kote duniani
Nakuomba kwa adabu, Mola wetu wa thamani
Mola Utupe sharabu, ya mapenzi ya imani

Mwalimu Mubaraka Nyamihasi
S. L. P 391, Tarime - Mara

KUZALIWA KWA BASHIRI

1 Bismillahi awali, kabla ya kubashiri
Yalazimu kila hali, jinale tulidhukuri
Muumba wetu Jalali, Jabbari Mutakabbir
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

2 Yatubidi tukubali, Ahmadi maqubuli
Aliifunga safari, aende Hoshiapuri
Kenda aombe kibali, kwa Mola Dhuljalali
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

3 Allah naomba kibali, maombi yaje kithiri
Isilamu kula hali, yahitaji jemedari
Asimame abashiri, waanguke wafedhuli
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

4 Rabbi ninasisitiza, dini ipo hatarini
Wapinzani waibeza, wanazusha ufitini
Uongo wanaukuza, kuipotosha imani
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

5 Dunia imekithiri, maovu bila ya soni
Dini nyingi utitiri, imetoweka imani
Watu mezidi kiburi, kukukana Rahamani
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

6 Aliomba na kufunga, sikuze arobaini
Machozi kulengalenga, akiililia dini
Ndipo Mola Mwenye anga, kamtokea sirini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

7 Labaika mja wangu, maombi nimekubali
Wewe ninakupa fungu, mwanao atawasili
Aje avunje miungu, amtukuze Jalali
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

8 Huyo ni mzao wako, jina lake ni Bashiri
Ni mtukufu kuliko, sifa zake ni kathiri
Atawavusha kivuko, watumishi wa Qahari
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

9 Ndani ya miaka tisa, atazaliwa mgeni
Haitopita kabisa, ni bishara ya Manani
Ndani ya wakati hasa, jinale Bashiruddini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

10 Ngome ataisimika, hodari wa kuhubiri
Jumuiyya itafika, na mataifa ya mbali
Watu wataelimika, utakuzwa ubashiri
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

11 Atafundishwa elimu, za dunia na za dini
Na awe mtaalamu, mjuzi wa Kuruani
Watashindwa mahasimu, watakaomfitini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

12 Nchi zitakombolewa, utakoma ukoloni
Wanyonge wa subiriwa, kutolewa utumwani
Mwana aloahidiwa, akiwa madarakani
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

13 Haya yalishatimia, ninayo waelezeni
Alfu na nane mia, nane na tisa mwanzoni
Bishara ilitimia, Februari ishirini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

14 Ukhalifa kaukwea, kaongoza waumini
Umma ukashuhudia, miujiza ya Manani
Tusome historia, mambo mengi tubaini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

15 Bishara ya kuzaliwa, ilipotimu mwanzoni
Masihi kaamriwa, asajili waumini
Na Marchi ikazaliwa, Jumuiyya ya Manani
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

16 Nyumba aliichagua, ya Sufi Hamadi Jalani
Baiat kapokea, hesabu ya waumini
Kiapo waloapia, watimu arobaini
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

17 Hatoambiwa tazama, kipofu asona mboni
Miujiza ya Karima, yule aso ibaini
Pengine ni madhuluma, muongozo hauoni
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

18 Wakati tumechegama, kwa mjumbe wa Manani
Wengineo wajitoma, kwa nguvu kumfitini
Kwa uwezo wa Karima, wameshindiwa njiani
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

19 Naufunga ukurasa, nakumbusha waumini
Ifikapo siku hasa, siku tuadhimisheni
Hutuba zenye hamasa, umma tulinganieni
Kuzaliwa kwa Bashiri, kulitimiza bishara

Mwl. Mubaraka A. Nyamihasi
S.L.P 391, Tarime - Mara

BURE MNANILAUMU

1. Bisimilahi Naanza, kwa jina lake Manani,
Napenda kuwaeleza, ndugu zangu waumini,
Yale ninayoyawaza, kutoka mwangu moyoni,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

2. Bure mnanilaumu, kosa langu silioni,
Nilofanya si adimu, vitabu vinabaini,
Au mumelamba sumu, dini mwaweka pembeni
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

3. Kuruani takatifu, maneno yake Raufu,
Yeye ni mkamilifu, Amejaa utukufu,
Kasema kimakinifu, tufuate bila hofu,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

4. Kasema kikamilifu, Kamuagiza rasua
Ya kwamba sitiehofu, Sheria zake murua,
wale walio na hofu, motoni wataungua,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

5. Muhamadi bwana wetu, yeye aliyetekeleza,
Akawaonyesha watu, kwa vitendo kupendeza,
Na kwa sisi zama zetu, ruhusa kuendeleza,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

6. Kama Wetu Muhamadi, yeye ametekeleza,
lweje wewe Saidi, lipi linakushangaza,

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

Bure nyie mwakaidi, amri za kupendeza
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

7. Mke ndugu nimeoa, naona nimewakera,
Lawama nyingi mwatoa, kwa maneno ya hasira,
Sheria mwaikosoa, hamuogopi akhera,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

8. Mke ndugu kumuoa, ni ruhusa ya Karima,
Hata kama umelea, hauna kosa kiama,
Lipi kosa onelea, bure mnanilaumu.,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

9. Rubuka zake sheria, zimewekwa kitabuni,
Nani wa kuzifatia, kama sio waumini,
Iweje twapuuziu, pale zinapobuini
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

10. Salaam nakuletea, shemeji Mbanga pokea,
Watu wananizomea, kimwali kujiolea
Sababu nimemlea, kinyaa wajionea
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

11. Na dada yangu Fatuma, nawe nakusogelea
Msangani yazizima , waona nimekosea
Kumbe mimi nimepima, halali kuonelea
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

12 Rajabu wa Mlandizi, hodi ninakupigia
Nakuomba uperuzi, sheria kufatilia
Ukiona huyawezi, Ngalombe muulizia,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

13. Hapa mahala tuliko, ni pagumu ndugu zangu
Mila twazipa mshiko, twayadharau ya mungu,
Ndugu zangu hukosiko, chonde turudi kwa mungu
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

14. Sisi tumeshazoea, kuyasoma vitabuni,
Au kutuelezea, toka kwa wana zuoni,
Na sifa twawazolea, kwamba walifata dini,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

15. Kwetu yanapotokea, dosari twazibaini,
Kwa bidii twazomea, bila ya hofu moyoni,
Jamii twaelekea, ya dini twaona soni,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

16. Wito wangu ninatoa, kwa wezangu waumini,
Mayatima kuchukua, kuwalea majumbani,
Tusisite kuwaoa, inapobidi hisani
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

17. Tusisite kuwaoa, pale inapolazimu,
Hisani kuwatendea, hilo ndilo la muhimu,
Thawabu tutazitoa, mbele ya mola karimu,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

18. Mola wangu mola wangu, dua natakabalia
Ni samehe mola wangu, kwa yaliyotangulia
Ni sitiri mola wangu, madhambi kunifutia
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

19. Usiniweke pamoja, kukosoa sheriazo,
Wanaozijenga hoja, kukejeli amrizo,
Mila zao wanataja, za dini kwao tatizo,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

20. Kwako ninakimbilia, nitazame mola wangu
Nasujudu kwa kulia, pokea maombi yangu
Madhambi kunifutia, sinikamate we mungu
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

21. Mola usinikamate, kwa yaliyotangulia,
Usinifanye kiwete, chonde chonde we Rabia,
Mimi kiumbe mtete, udhaifu najutia,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

22. Ni samehe mola wangu, dhambi kuniondolea,
Shetani asije kwangu, mabaya kuniwekea,
Sheriazo mola wangu, mimi ninazitetea,
Sijamkosea mungu, bure mnanilaumu.

Mwl. Ali Ng'ambage
Njinjo Kilwa

Bukkede Afrika

Kutoka uk. 5

hesabu uone binadamu huyu alikuwa amepata kiasi gani cha pesa kwa mwezi! Dhulma ilioje! Wengine wanatumbua na wengine wazidi kukondeana! Hilo ndilo onyo la Khalifa wa Mwenyezi Mungu.

Mwaka 1972 alijitangaza kuwa Rais wa maisha, na cheo hicho akaona ni kidogo ndipo mwaka 1977 akajitangaza kuwa Mfalme. Kifuani pake wakati wa kuapishwa kuwa Rais alivaa medali 48 na mbili ndizo zilikuwa halali, kwani alikuwa amezipata kutoka kwa Wafaransa wakati akipigana huko Vietnam.

Jambo la kuhuzunisha na kutia uchungu ni kwamba wakati umoja wa mataifa ukilihesabu taifa lake kuwa miongoni mwa mataifa 25 yaliyo taabani kwa umasikini, Mfalme Jean Badel Bokassa alikuwa na majumba matano ya kifahari nchini, jumba la kifahari kwenye Riviera -Ufaransa na jumba jingine huko Vila nchini Switzerland.

Kana kwamba hiyo haitoshi alikuwa na majumba ya kifahari katika sehemu zote za Jamhuri na magari mengi ya kifahari.

Uchu wake wa mali na madaraka vilikuwa bado havijashibishwa. Mwaka 1977 alitangaza nchi yake kuwa ni Falme na akajitangaza yeye kuwa ndiye Mfalme wa nchi hiyo. Mara baada ya kujitangaza kuwa Mfalme, matangazo kabambe yalifanyika. Katika kila pembe ya jiji la Bangui aliweka sanamu yake kubwa. Hiyo ilikuwa ni bashrafu tu, makubwa zaidi yalikuwa yanafuata.

Kuapishwa kwake kulifuata mtindo uleule wa Napoleon aliyoutumia mwaka 1804, gari la wazi lilitengenezwa huko nchini Ufaransa katika mji wa Nice, na gari hili lilitengenezwa mithili ya ndege aitwaye 'tai'. Majoho yake yalinakishiwa na vito vya thamani, sare kama ya Napoleon ilitengenezwa na askari 5000 wote hao walitengenezewa sare zao. Na hiyo yote ni gharama kwa mtoa kodi wa nchi hiyo.

Mkewe alivaa gauni iliyonakishiwa na dhahabu na vito vingine vya thamani, lakini kilele cha ujahili wa Bwana huyu ni wakati alipoweka katika taji lake la kifalme vipande 2000 vya almasi. Kwa ubadhirifu huu na ujahili usio na mfano hata Papa wa Kanisa Katoliki ambaye alikuwa amealikwa ili kumuapisha Mfalme huyo alishauriwa kuwa mbali na aibu hiyo. Hivyo hakufika. Na Jean Badel Bokassa alitabasamu na kusema kilichomshinda Papa mimi nakiweza! Hivyo akajiapisha yeye mwenyewe.

Sherehe zote hizi za kukata na shoka zilifanyika kwenye uwanja wa wazi ambapo waliendelea kutokwa na jasho, baadae walikaribishwa kwenye jumba la Mfalme kwa ajili ya dhifa. Masikini wote walikwishaondolewa barabarani ili wasichafue mandhari. Wakati wakielekea kwenye jumba la Mfalme walipita kwenye makaburi ambapo watoto walikuwa wamezikwa kwani katika nchi hiyo mtoto mmoja katika watano alifariki kabla hajafikisha mwaka wake mmoja wa kuzaliwa. Hayo yote hayakuumiza roho za hao viumbe pamoja na Mfalme wao. Huko nyumbani kwa Mfalme waliendelea na sherehe iliyohudhuriwa na waalikwa 5000. Hao walikula na kunywa. Chupa moja ya mvinyo ikiwa bei ya paundi 70. Chupa 24,000 za Shampeni zilinywewa zilizogharimu paundi 200.

Hao ndio viongozi tuliowapata katika Afrika. Wanavimbiwa wakati sisi tunalala njaa, wanatia vidudu mtoni na sisi tunaambulia marapurapu na mitumba, wakipata mafua tayari wanapelekwa kwa wale waliokuwa wanatutawala kwa ajili ya matibabu! Madini yetu yanauzwa kwa 'thamanan kalilan' wanashindwa uchaguzi wanalazimisha kwa wizi na vitimbwi. Watu wanapoteza maisha yao, gharama iliyotumika kwenye uchaguzi inakwenda bileshi. Katiba zinabadilishwa ili watawale dawamu. Safari zisizokwisha na ujumbe mzito pesa za kutosha vitanda kadhaa hospitalini zinapotea bure. Tume asubuhi na jioni, tena nyingine wala hazina maana. Kiongozi kajikwaa kidole gumba, tume! Mkufu wa bibiye umepotea, tume! Tume hadi inakuwa tume ya miradi. Mwisho wa tume moja matayarisho kwa tume nyingine! Mishahara minono na marupurupu kibao. Vijana wanakalia mawe madarasani katika karne inayosemwa kwamba ni ya sayansi na teknolojia. Mabingwa mno wa kutafuta fimbo, wakati tumekwishaumwa na nyoka. Mara nyingi watu hushikwa na kigugumizi hawa ni wakombozi au wezi? Na mwizi nyumbani kwake wapi? Kwa mtaji huo Afrika itaendelea? Jibu unalo wewe mwenyewe.

TANZIA

Mzee Ibrahim R. Mkoga hatunaye

Kwa masikitiko, tukiwa tunakwenda mtamboni tumepata taarifa kwamba Mzee Ibrahim Mkoga amefariki dunia usiku wa kaumkia Ijumaa tarehe 23/3/2012 na kuzikwa mchana wake baada ya sala ya Ijumaa huko Mkongo, Rufiji Mkoa wa Pwani. ***Inaa lillaahi wainnaa ilayhi Rajiuun.***

Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi - Amin

Maelezo kamili ya maisha ya Mzee Mkogas yatatotolewa toleo lijalo. Inshallah.

AHMADIYYAT - ISLAM YA KWELI IMENITENDEA / IMETUTENDEA NINI?

- **Ahmadiyyat - Islam ya kweli imetupa imani katika Mungu Aliye hai Ambae husikia na hujibu. Kupitia Kwake tumepokea zana ya kutegemewa zaidi kwa mwaminio, yaani, nguvu ya sala - Silaha ya maombi.**

- **Ahmadiyya - Islam ya kweli imetuwezesha kutambua ukubwa wa daraja la bwana wetu mpendwa, Hadhrat Muhammad Mustafa (saw), Khatamman Nabiyyin, Muhuri wa Manabii.**

- **Ahmadiyyat - Islam ya kweli imetupa utambuzi wa Imam wa zama, Nabii Mfuasi (as) wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw)**

- **Ahmadiyyat - Islam ya kweli imetupatia umoja kwa njia ya Ukhalifa, taasisi yenye baraka zaidi katika Islam.**

- **Ahmadiyyat - Islam ya kweli imetupa shauku ya kuitumikia Islam na utashi wa kujitolea katika njia ya Islam.**

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MAWAIDHA YA MWISHO

Lahore si kwetu. Kwetu ni Bhera, na sasa ni Qadian. Nawaambieni, mtu yeyote mjni Lahore hakupinga *Ukhalifa* wangu wala hawezi. Msimfikirie vibaya yeyote. Kama mmeamini, mshukuruni Mungu; waila jitahidini kupata uthabiti. Ijapokuwa naugua na kusimama kwangu ni shida, hata hivyo nachukua nafasi hii ili kusisitiza kuwahakikishieni kwamba *Ukhalifa* si jambo hafifu la kuchezea. Hamwezi kunufaika na ubishi huu. Hakuna atakayewafanyeni *Khalifa*, wala yeyote hawezi kuwa *Khalifa* katika uhai wangu. Nikifa, yule tu atakuwa *Khalifa* ambaye Mungu Mwenyewe Atamfanya. Mmefanya baiati kwangu, msiwaze kujichukulia daraka la *Khalifa*. Mungu Amenifanya *Khalifa* nami siwezi kuondolewa kwa amri yenu, wala hamna yeyote mwenye uwezo wa kuniondoa. Kama mkijidai sana, basi tambueni kwamba ninao Ma-Khalid bin Walid watakaowaadhibuni kama waasi waadhibiwavyo.

Sikilizeni! Maombi yangu hufikia Arshi, na Mola wangu Hutimiza mipango yangu hata kabla sijamwomba. Kunikaidi ni kumkaidi Mungu. Basi komeni na tubuni. Subirini kwa kitambo; kisha yule atakayenifuata atawatendeeni kama Apendavyo Mungu.

Baadhi ya mambo ambayo mnahitilafiana yamekwisha fafanuliwa tayari na Hadhrat Mirza Sahib a.s. Yule aendaye kinyume cha kauli yake si Ahmadiyya. Juu ya mambo asiyoyaeleza maoni yake, nyinyi hamna ruhusa ya kuyafikiria-fikiria pasipo idhini yangu. Basi zuieni kalamu zenu na ndimi zenu kuhusu hayo mpaka *Khalifa* ayataje, ama *Khalifa* wake adhihiri. Msidiriki, basi, kupiga domo juu ya mambo ambayo Imam na Kiongozi wetu amenyamaa kuhusu hayo, la sivyo maandiko yenu yatakuwa bure. Hamwezi kutoa udhuru kwamba mnalazimika kushika kalamu zenu kwani mimi situmii kalamu yangu. Someni vitabu vyangu *Nuruddin*, *Tasdiq Barahine Ahmadiyya*, *Faslul Khitab*, *Ibtal Uluhiyyate Masihi*, mjue kwamba naelewa sana kuandika. Nimezuiwa na hekima ya Mungu tu; naam, kwa hakika ni Mungu Aliyenizuia.

Nawasihini mara nyingine. Angalieni umri wangu na maradhi yangu. Kisha fikirini kwamba je, mabishano yenu yatawasogezeni karibu na Mungu? Kamahapana, basitegeni masikio kwa ninayowaambieni na kuzeni mapenzi baina yenu. Basi onyesheni adabu nzuri ili niridhike jinsi nilivyopendezwa na kuona msikiti huu katika ziara yangu ya mji huu. Mungu na Ajaalie kwamba nikiondoka nisikie mmekuwa kitu kimoja na mnapendana. Daima yakimbilieni maombi. Mimi nami nitawaombeeni."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. mara nyingi alieleza tukio moja lifuatalo lililokuwa mfano maalum wa njia yake ya kuhojiana: "Sheikh mmoja asiyekuwa Ahmadiyya alinialika kwenye chakula cha mchana. Nilipowasili nikakuta amemwalika pia Sheikh mwingine asiyekuwa Ahmadiyya aliyekaa pamoja nami. Akaongea nami kwa upole juu ya mambo ya dini. Alieleza kwamba anaamini Nabii Isa alikufa kifo cha ajali, alimheshimu Hadhrat Mirza Sahib a.s. kuwa mtu mkweli, na alikubaliana naye katika mambo yote, na alikuwa kama mwanafunzi wake, lakini akataka kuniuliza jambo moja dogo. Namfikiriaje yule asiyekubali madai yake? Nikamwambia: Kuna njia rahisi ya kujibu swali hili. Tunaye Musa a.s., na tunaye

Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu na tena tuna Masihi wa silsila ya Musa a.s. na Masihi wa silsila ya Kiislamu. Unatambua utamfikiria nini anayemkataa Musa a.s., na pia wajua utamfikiria nini anayemkana Muhammad s.a.w, Mjumbe wa Mungu. Sasa, jinsi utakavyomfikiria anayemkataa Masihi wa silsila ya Musa a.s. ndivyo utakavyomfikiria anayemkataa Masihi wa Kiislamu. Aliposikia hayo, mwenyeji wetu akamwita mwanaye na kumwambia: Lete chakula haraka; si jambo rahisi kuhojiana naye."

Mnamo Julai 25, 1912, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliweka jiwe la msigi wa Talimul Islam High School akinena:

"Nimewahi kusoma mahali fulani ya kwamba kama waaminio arobaini wakiomba pamoja, dua yao hupokelewa na Mungu kwa fadhili yake. Wakati huu tumejumuika hapa zaidi ya arobaini. Baadhi yetu pengine wamekwisha fanya kosa fulani. Hao wapaswa kutubu na kuomba msamaha. Kisha tutaomba pamoja ya kwamba Mungu Mtukufu Apendezwe kwa kutayarisha katika shule hii watumishi waongofu wa dini na kwamba Awaweke mbali na shule hii wenye moyo mwovu wawezao kuwapotosha wengine; na kama mmoja wao apate kuingia humu, Yeye Amwezeshe kutubu kweli kweli. Shabaha ya shule hii ni kwamba wataalamu watawa na wema watokee katika shule hii."

Kisha wote waliokuwapo wakaungana nanaye katika maombi ya kimya. Hadhrat Khalifatul



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masihi I r.a.

Masihi r.a. akaulizwa na Sheikh mmoja asiyekuwa Ahmadiyya: Je, Hadhrat Mirza Sahib alikuwa mtaalamu mkubwa wa elimu ya dini? Kajibu:

"Yeye hakuwa mtaalamu katika maana hii kwamba alijisomea katika Chuo Kikuu cha dini. Baba yake alimwajiri Sheikh mmoja wa kishia wa Batala aitwaye jina Gul Ali Shah kama mwalimu wake alipokuwa kijana. Lakini

Mwenyezi Mungu Akamjaalia utaalamu wa hali ya juu hata kwamba masheikh wa India na Uarabu hawakuweza kuleta mfano wa vitabu vyake kwa lugha ya Kiarabu. Aliamini sana katika dua, na Mungu Akimpokelea maombi yake Akamjaalia ujuzi wote uliotakikana."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliamini ya kwamba hali hiyo ya utaalamu itakuwa ya Mwana Aliyeahidiwa wa Hadhrat Mirza Sahib a.s., Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad ambaye alieleza habari za kujifunza kutoka kwake:

"Nilijifunza Qur'an Tukufu kutoka kwa Hadhrat Khalifatul Masihi I r.a. katika muda wa miezi sita. Kwa kuwa koo langu lilikuwa dhaifu, hakuniruhusu kusoma matini yake. Yeye mwenyewe aliisoma na kuitafsiri, nami nikasikiliza tu. Kisha akatoa maelezo ya baadhi ya sehemu za muhimu kwa midomo na akamaliza katika mwezi mmoja. Nilihudhuria katika darasa lake la Qur'an Tukufu lililokuwa kwa watu wote, lakini hayo tu ndiyo aliyonifunza. Kisha akanisomesha kitabu cha Hadithi za Mtume s.a.w. zilizokusanywa na *Bukhari*, katika miezi mitatu. Hafidh Raoshan Ali r.a. akaungana nami katika masomo hayo. Yeye alikuwa mfahamivu na mara nyingi aliuliza maelezo kadha wa kadha. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akatoa maelezo. Mara moja au mara mbili mimi pia niliuliza swali. Nikajibiwa. Mara ya tatu nilipouliza swali, akasema: Mian, Bwana Hafidh ni Sheikh, anauliza nami najibu. Lakini sitajibu maswali yako. Yote niyajuayo nakueleza; siwezi kukuambia nisiyojua. Umtumishi wa Mungu, na mimi kadhalika. U mfuasi wa Muhamad s.a.w., nami kadhalika. Kuitetea Islam si kazi yangu mimi pekee, ni yako pia. Wapaswa kutafakari na kutafuta majibu. Usiniulize. Hapo baadaye sikumwuliza tena maswali. Nafikiri hilo lilikuwa somo lenye thamani ya juu sana alilonifundisha."

Vipi mtu aweza kuepukana na dhambi, ni swali ambalo jibu lake Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliwauliza watu wengi mashuhuri. Jawabu la Maulana Muhammad Qasim Nanautwi lilikuwa:

"Kukikumbuka kifo kwamkinga mtu na dhambi."

Tiba iliyopendekezwa na Shah Abdul Ghafur Mujaddidi ilikuwa:

"Mtu anayemtanguliza Mungu moyoni mwake hulindwa na dhambi."

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema:

"Kufululiza kuomba kuzuia maelekeo kwenye dhambi (*Istighfar*) ni kinga kwa kujilinda na dhambi."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alifikiri kwamba kukaa na watu wema na kuomba daima pia ni tiba za kufaa. Kwa ajili yake mwenyewe, safari moja akajaribu nji hii ya kwamba aliweka Qur'an Tukufu mahali alipoweza kuiona saa zote, ili aweze kujisihi mwenyewe: 'Unakiamini Kitabu hiki, hata hivyo waelekea kukiasi.' Hiyo ikamzuia hata kwamba wazo hilo likamtoka moyoni mwake. Aliona njia hizo zote zinasaidia. Baadhi yao wanaathirika na njia hii na wengine wanaathirika na nyingine. Jambo kubwa zaidi ni kwamba mtu adumu kutia bidii hadi ufaulu upatikane.

Mkutano wa Mwaka wa 1912 ulifanyika tarehe 25-27 Disemba. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akiuhutubia Mkutano alinena:

"Uhusiano wa mtu unapoendelea kusonga mbele, Mungu Anamwagiza Jibrili a.s. kuimarisha uhusiano naye, basi mtu huyo anaanza kujifaidisha kutokana na malaika. Tajiriba kama hizo zinaanza kuwa kwa nadra. Nasema kwa uthabiti si kwa kujikweza, majivuno au kiburi, bali kwa kutoa mfano tu wa fadhili ya Mungu, ya kwamba nimewaona malaika hao, nao wamenisaidia namna ambavyo haiwezi kufahamika. Wakaniambia nizingatie namna wanisaidiavyo."

Akataja mifano ya ufaulu usio wa kawaida waliopata masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w., kwa kueleza manufaa ya kukaa na watu wema, na akakazania kufafanua baraka za utii na kujitupa kwa Mungu. Mzingatie wajibu wenu kumhusu Mungu kwa kila jiha, saa zote maishani mwenu, ili kifo, wakati wowote kikiwafikieni, kiwakuteni katika hali ya utii mkamilifu kwa Mungu. Ishikeni kwa imara, nyote pamoja, kamba ya Mungu wala msifarakane (3:103,104). Akasihi kukuza kupendana, kupatana na kuungana pamoja, na akasisitiza kubeua uadui, ukinzani na mafarakano.

Akamalizia kwa kusema:

"Watu wa dunia waliponiambia: Tumekufanya mkuu wetu, posho yako kila mwezi iwe kiasi gani? Nikaelekea kwa Mungu na kumwomba: Mola wangu, Hujanifanya abadan nimtegemee yeyote. Je, sasa ninapoelekea mwisho wangu Utanifanya niwategemee viumbe vyako? Yu Mkarimu sana kwangu, Akanipatia kutoka pale nisipoweza kufikiria. Nawaambieni tu: Itangulizeni imani yenu juu ya dunia; epukaneni na pupa, ulaghai na fitina."

Disemba 27 ilikuwa siku ya Ijumaa. Katika hotuba yake ya Ijumaa akasema:

"Msikiti huu (Masjid Nur) unachukua jina langu, likini ni mdogo. Yafaa upanuliwe, lakini kwa kuzagaza wema. Anzeni shule humu ndani yake kwa kufundisha Qur'an Tukufu. Talimul Islam School ina jengo zuri, inapata fedha kutoka serikali na inaangaliwa vizuri; lakini hakuna anayetunza Madrasa Ahmadiyya ambayo haiangaliwi. Niliwaelekeza kwenye hiyo, na kamati moja iliundwa, lakini kwa vitendo hakuna kilichotendeka."

Hafidh Raoshan Ali r.a., mwanafunzi mkuu wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alieleza ya kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa ameandika katika daftari ya ukumbusho baadhi ya faida alizopata kwa sababu ya kukaa Qadian. Mojawapo ilikuwa:

"Kabla sijahamia Qadian nilitia bidii yote kufaulu kupata kwa uchache rafiki mmoja atakayenipenda kwa ajili ya Mungu tu pekee, nami nikatumia maelfu ya rupia katika utafutaji huo lakini sikufaulu. Nilipofika Qadian, Mwenyezi Mungu Akanijaalia jamii nzima ya marafiki ambao roho yangu ilikuwa na kiu yao, tena sikutoa hata peni moja.

Faida nyingine niliyopata kwa kukaa na Hadhrat Mirza Sahib a.s. ilikuwa kwamba mapenzi ya dunia yalijifia kabisa moyoni mwangu. Chunguzeni kila jiha ya maisha yangu. Je imo hata chembe ya mapenzi ya dunia ndani yangu? Hiyo yote ni neema ya usahibu mtukufu wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. Kuna methali inayojulikana sana: Mapenzi ya dunia ni chanzo cha kila hatia. Nimejipatia manufaa kutoka kwa usahibu wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. ambayo ndiyo shabaha ya mafundisho ya Mungu, ni chanzo cha wokovu na yaleta maisha ya kimbinguni katika dunia hii hii."

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Semina ya Malezi kwa Khuddam na Atfal yafana Nachingwea - Lindi



Sadr Khuddamul Ahmadiyya Bw. Ali Khamisi Mbambwa (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Khuddam na Atfal waliohudhuria semina katika tawi la Nachingwea Mkoani Lindi.

Semina ya malezi (Tarbiyyat Seminar) ilifanyika mnamo tarehe 11/02/2012 jumamosi katika Jamaat ya Nachngwea Mjini Mkoani Lindi. Katika semina hiyo Khuddam wapatao 35 na na Atfal 53 wa Jamaat za Nachingwea, Farm 17, Jamaat ya Libea na Marambo waliweza kushiriki.

Semina ilifunguliwa kwa usomaji wa Qur'an Tukufu ambayo ilisomwa na Mwl. Mussa Rashidi kutoka Jamaat ya Farm 17. Pia lilifuata shairi tamu lililosomwa na ndugu Yusuf Saidi kwa uhodari mkubwa.

Kabla ya kiapo cha Khuddam na Atfal kilichoongozwa na Sadr Khuddamul Ahmadiyya -Tanzania (Bw. Alli Hamisi Mbambwa), kijana Fadhili Jamali na Yusuf Ahmad walipata fursa adhimu ya kusoma hadithi arobaini za Mtume (saw). Ama hakika Hadithi hizo ni bahari ya elimu na maarifa katika maisha yetu siku zote.

Ndipo baadaye risala iliyoandaliwa na Khuddam wa matawi hayo ilisomwa na kijana Hassan Seif mbele ya mgeni rasmi.

Hotuba ya ufunguzi rasmi wa Semina hiyo ilitolewa na Mgeni Rasmi Bw. Saidi Kalindima ambaye ni Rais wa Jamaat Ahmadiyya mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika hotuba yake ya ufunguzi aliweza kutoa nasaha zake kwa vijana (Khuddam na Atfal). Pia alieleza kuwa tumewacha shughuli zetu za kidunia kwa ajili ya semina ile ya malezi. Hivyo aliwaomba vijana waelekeze mawazo na fikra zao kwenye mafunzo ya semina.

Aidha Rais aliwaeleza vijana (Khuddam na Atfal) kuwa kulingana na umri walio nao, wao wana fursa nzuri ya kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu, kwa maana katika kipindi cha ujana ndipo tunakuwa wenye nguvu na afya njema ya kutuwezesha kutekeleza malengo mbalimbali tunayojiwekea. Lakini pia aliwatahadhirisha vijana kuwa ni katika umri huu ambapo hukutana na changamoto mbalimbali za kimaisha. Hivyo aliwataka Khuddam wawe mstari wa mbele katika shughuli za ibada ili pia wadogo zao (Atfal) waweze kuiga mfano kutoka kwao.

Baada ya hotuba hiyo ya mgeni rasmi, Qaid wa Jamaat ya Nachingwea Mwl. Ally Mmoto aliweza kutoa nasaha zake. Katika nasaha zake alieleza kuwa, vijana ni muhimu tufahamu kuwa kila mmoja wetu ni kiongozi, hivyo ni lazima vijana tuwe katika mstari wa mbele katika kujifunza nidhamu mbalimbali za Jamaat na kuzitekeleza kikamililfu. Aidha aliwataka Khuddam kuwapa mafundisho bora Atfal kwani wao ndio khuddam wa kesho.

Akitoa hotuba kwenye semima hiyo, Sadr Khuddamul Ahmadiyya nchini Bw. Alli Hamisi Mbambwa alisema; vijana ni muhimu watambue na watekeleze majukumu yao ipasavyo kwa kuwa wao ndio uti wa mgongo wa Jamaat. Vijana ndio wenye nguvu ya kuchapa kazi na hivyo kuweza kuleta maendeleo ya Jamaat na nchi kwa ujumla. Aidha aliwaasa vijana kutanguliza shughuli za dini mbele ya dunia kwa kuwa shabaha ya kuumbwa kwetu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Mola wetu.

Hotuba juu ya nidhamu ya Jamaat ilitolewa na Bw. Mussa Rashidi. Katika hotuba yake alieleza umuhimu wa utii kwa viongozi wa Jamaat. Alisema kuwa hii ni Jamaat ya kiroho hivyo ni lazima mienendo yetu ijali zaidi Taqwa -ucha Mungu ambao ndio wajibu wetu mkubwa.

Kipindi cha chemsha bongo kilifuata ambacho kiliongozwa na Bw. Ally Mmoto Qaid wa Khuddamul Ahmadiyya wa Jamaat ya Nachingwea.
Rais wa Jamaat ya Nachingwea Bwana Yusuf Mmoto, pia alipata fursa ya kutoa hotuba katika semina hiyo. Yeye aligusia zaidi umuhimu wa kumtegemea Mwenyezi Mungu. Alinukuu kutoka maandiko ya kiongozi wetu mpendwa muanzilishi wa Jamaat hii Tukufu Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema; "Mimi sijapewa silaha yoyote zaidi ya kumtegemea Mwenyezi Mungu". Hivyo rais alitumia fursa hiyo kuwataka vijana kufanya mabadiliko chanya ya maisha yao kulinga na nasaha mbalimbali zilizotolewa kwenye semina hiyo.

Kwa upande wake Mwalimu wa Jamaat ya Nachingwea Mwl. Mustafa Mambo aliwahutubia vijana kwa kueleza umuhimu wa kufanya mabadiliko ya kikhulka na kujitahidi katika shughuli za Jamaat. Pia aliwataka vijana wajitahidi kutekeleza ibada mbalimbali za Jamaat kama vile sala na kutoa michango ambayo ni muhimu sana katika maendeleo yetu ya kiroho.

Hatimaye Mgeni rasmi alitoa hotuba ya kufunga semina hiyo. Katika nasaha zake za mwisho aliwaomba vijana na washiriki wote wa semina ile watafakari kwa kina juu ya mafunzo yaliyotolewa na kumuomba Allah ili Awawezeshe kufanya mabadiliko mema katika maisha yao. Kisha alitumia fursa hiyo kuongoza maombi ya kufunga semina hiyo.

Morogoro yarindima kwa Mahubiri

Na Nur ud Din Yusuf Athumani
Kambaulaya
Morogoro.

Bwana Hamisi (Beta King), kama ilivyo kawaida yake ya kufanya mahubiri bila ya kuchoka, aliandaa kipindi cha maswali na majibu katika kijiwe cha kahawa cha Bwana Dudus. Sheikh Adnan, Mbashiri wetu wa Canada alihudhuria pia katika siku za mwanzoni za kikao hicho na kuongeza mvuto wa vikao hivyo. Baada ya siku chache vikao vya aina hiyo hiyo vikafanyika tena kwenye kijiwe kingine cha kahawa jirani na eneo hilo, kwenye kiwanja cha mzee wetu marehemu Abubakar Hasan. Maswali kadhaa yalijibiwa na majibu maridhawa yalitolewa.
Kiwanja hicho kimekaa kwenye sehemu nzuri ya kona ya mtaa wa Karume na Dedan Kimathi na kipo katikati ya jiji la Morogoro kikiwa kimezungukwa na majumba ya kale ya eneo hilo muhimu la Karume. Mara moja likatujia wazo la kufanya mhadhara kwenye kiwanja hicho ili wengi wa watu wapate kufaidika kwa njia ya vipaza sauti vitakavyoweza kufikisha sauti hata kwa wale wanaozuiwa na Masheikh wao kuhudhuria.
Mjane wa bwana Abubakar alitoa kibali cha kiwanja hicho kitumike kwa mikutano ya dini ya Jumuiya na kibali hicho kikapitishwa na mwenyekiti wa mtaa wa Karume na hatimae kuambatanishwa na barua ya kuombea kibali kwa mkuu wa Polisi wa wilaya ya Morogoro. Kibali kikapatikana kwa haraka sana na mara mhadhara ukaanza.
Wengi walivutiwa na mawaidha mazuri yaliyokuwa yakitolewa na wanazuoni wa kiahmadiyya wakiwemo sheikh Ahmad Daud Mmoto, Sheikh Karimuddin Shams, Mwalimu Musa, Mwalimu Shamuun, Ustadh Rajab na sheikh Bakri Abedi Kaluta. Habari za kuwa nabii Isa a.s. ameshafariki dunia na kuzikwa huko Kashmiri India badala ya kuwepo mbinguni ziliwashangaza wengi. Ushahidi uliotolewa ndio ukawa gumzo la vijiwe vya Morogoro na kuzaa mijadala mingi ya vijiweni kati ya mashabbik na wale waliotuelewa. Habari za Hadhrat Ahmad a.s. kuwa ndie yule Isa a.s. anayesubiriwa na Waislamu kwa Wakristo zilitoa pia misisimko ya aina yake kwa Waislamu na Wakristo.
Vipindi vya maswali na majibu ndio vilileta msisimko mkubwa zaidi pale watu waliporuhusiwa kuuliza maswali na majibu mwanana yakawa yakitolewa na wanazuoni wa Kiahmadiyya. Watu wote wakiwemo Masheikh na Mapadri walialikwa kuja kuuliza maswali na hata kutoa hoja sawa na mitazamo yao. Siku ya siku wanazuoni toka kwenye taasisi ya mihadhara ya Al Malid wakaibukia uwanjani hapo na kuomba kufanya mjadala nasi. Walipopewa tu kipaza sauti wakajitangaza pamwe na kuitangaza dhamira yao ya kutaka mjadala. Punde si punde uwanja ukajaa kupita kiasi na msisimko mkubwa ukazuka na shangwe za Takbir zikawa zikisikika toka kwa mashabbik wa Al Malid waliokuwa wakihamasishwa hivyo na wahadhiri wao.
Mjadala ukaahirishwa hadi siku iliyofuatia na kamanda wa mapambano wa siku hiyo kwa upande wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya alikuwa Mwalimu Abdallah Mbanga ambaye alitoa hoja madhubuti sana

Endelea uk. 10

Morogoro yarindima kwa Mahubiri

Kutoka uk. 9

zilizowastaajabisha watafutao ukweli na kuwatia kiwewe wapinzani na mashabiki wao, ambao baadhi yao walishindwa kujizuia na kuzua tafrani ya kukata kwa shoka. Ustadhi fulani wa Answar Sunna aliyekuwa amekiremba vizuri kidevu chake kwa ndevu zilizochanwa vizuri na kuachiwa ziteremke hadi kifuani, alitoa burudani ya aina yake pale alipotaka kuwavaa waahmadiyya kwa vipigo vya karate vya huu haa....Nguvu ya ziada ilibidi kutumika kumdhibiti mbabe huyo na ni msaada tu wa Allah kwamba hakuna aliyewahi kuvunjwa mbavu zake kwa kipigo cha mbabe huyo. Tafrani ilikuwa kubwa na kusababisha gari ya polisi iwahi hapo mara moja ili kudhibiti hali ya mambo. Wakati inawasili gari hiyo Waahmadiyya wote walikuwa wameshaondoka baada ya kuamriwa hivyo na uongozi wao kuwa Waahmadiyya wote waondoke mara moja. Watu wakawa wamegawanyika katika makundi madogo madogo wakitafakari na wengine kujadiliana na kutoa rai mbali mbali za mada na tafrani zilizojiri.

Msikiti wa jirani wa Answar Sunna ukaamua kutumia vipaza sauti vyake kutoa mawaidha dhidi ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya na kuutangazia umma kuwa, Mungu Apishe mbali, Jumuiya ya Ahmadiyya inajihusisha na biashara ya mihadharati. Siku zilizofuata, wakati wahadhiri wa Kiahmadiyya wakitoa mawaidha yao yaliyokuwa yakirembwa kwa aya za Qurani na kauli za Mtume s.a.w. na huku wakihamasisha amani na upendo miongoni mwa jamii, gari la Redio Imani likasogea mbele ya kiwanja cha mhadhara wa Ahmadiyya, likiwa limesheheni vipaza sauti vyenye nguvu sana na kupeperusha hotuba ya sheikh wao aliyekuwa amejifungia msikitini akitoa mawaidha yenye kashfa dhidi ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Kashfa za aina hiyo ziliendelea kwa takriban siku tatu hivi lakini zikasimamishwa ghafla baada ya kuonekana kuwa watu wanavutiwa mno na waahmadiyya kutokana na uvumilivu wanaouonyesha mbele ya kashfa nzito kama hizo bila ya kujibu mapigo ya kashfa hizo. Bwana fulani alitamka kwamba Waahmadiyya nimewapa maksi mia kwa mia kwa kuendelea kutoa mawaidha ya Qurani bila ya kushughulika na matusi yaliyokuwa yakitolewa mbele yao. Watu wakaanza kuwalaani Answar Sunna kwa mwenendo wao huo ambao haukuonyesha kulingana na maadili yoyote ya Islam.

Baada ya kupita kama siku kumi hivi ya tafrani hiyo, uongozi wa Al Mallid ukaja na ombi la kufanya nasi mjadala katika mhadhara wao kwenye uwanja wa Mlapakolo. Wakatoa ahadi ya kudhibiti fujo na tabia zisizo za kistaarabu.

Ombi lao lilikubaliwa na mnamo tarehe 13 Februari, 2012 Mjadala wa kukata na shoka ukafanyika kwenye viwanja vya Mlapakolo, mbele ya nyumba ya Sheikh wa Wilaya ya Bakwata, Sheikh Kairo. Matangazo makubwa yalifanywa na taasisi ya Almallid kuwaomba watu wahudhurie kwa wingi kwenye Mjadala huo, matangazo yalifanywa mitaani na misikitini.

Mamia ya watu walihudhuria kwenye mjadala huo uliobeba mada ya kifo cha nabii Isa a.s. Al Mallid walishindwa kuleta hata ayamoja au Hadithi ithibitishayo kuwa Isa a.s. bado hajafa na atarejea duniani. Mwanzoni walianza kwa uadilifu katika kupeana muda wa mijadala na kukawa na Mwenyekiti katika kila upande, ambapo upande wa Ahmadiyya Sheikh Karimuddin Shams akawa ndie Mwenyekiti. Mwishoni uzalendo ukawashinda na kuamua kumpa mhadhiri wao fulani muda usio na mpaka, kinyume na makubaliano, na akautumia vema muda huo kwa kutema cheche dhidi ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Hatimaye waahmadiyya wakaamua kufungasha na kuondoka katika eneo la mjadala. Hali hiyo ikasababisha kutoweka kwa mvuto wa tamasha hilo na hivyo watu wakaanza kusambaa.

Hali hiyo ilisababisha Waahmadiyya wasirejee tena kwenye hafla hiyo na Al Mallid wakajikuta wanapata watu wachache sana wanaohudhuria kwenye mhadhara wao. Sheikh wa Wilaya aliwalaumu sana kwa mwenendo walioutumia dhidi ya Waahmadiyya na akawashauri kuwa hawataweza tena kupata watu katika mihadhra yao hadi wakawaombe radhi Waahmadiyya na kuwaomba wakubali kuendelea tena na mjadala.

Walipokuja kuomba radhi na kuomba tuendelee na mjadala, walishangazwa kuona ombi hilo limekubaliwa bila msito wowote. Mjadala ukaendelea kwa siku tatu kuanzia tarehe 17 hadi 19 Februari 2012 na kukusanya kundi kubwa la watu. Watu wengi walikiri kuwa kwa mara ya kwanza wameweza kufahamu madai ya Waahmadiyya kwa kina baada ya mijadala hiyo. Wengi wamevutiwa na baadhi yao wameahidi kujiunga na Jumuiya.

Mijadala ikaendelea tena kwa siku mbili za tarehe 21 na 22 Februari 2012 kwenye viwanja vya Mwembesongo ambapo idadi ya waliohudhuria ilikuwa ni mara mbili zaidi ya wale waliohudhuria Mlapakolo. Kwa hakika ujumbe wa Ahmadiyya umeenea sana ndani ya siku hizo na baadhi ya watu wanaonyesha ukaribu na Jumuiya baada ya picha halisi ya Jumuiya kuwadhihirikia kadamnasi.

Ufuatiliaji wa waliovutiwa na Ahmadiyya unaendelea na huku Masheikh walio wapinzani wa Jumuiya wakiendelea kuungua ndani ya moto wa hasira na ghadhabu zao za husuda.

Maandalizi ya Ijtimaa 2012

Khuddam na Atfal wanatangaziwa kuwa Ijtimaa yetu itafanyika tarehe 15,16 na 17 Mwezi Juni 2011 Kitonga - Dar es salaam.

Mashindano kwa Khuddam:

1. Hifdh-ul-Qur'an (Kuhifadhi Qur'an) Juzuu ya 28, Juzuu ya 29 pamoja na Juzuu ya 30

2. Qur'an Tukufu Tafsiri: Al-Kahf 1 - 13: Sura 24: 56

3. Kutoa Hotuba: Umuhimu wa Sala

4. Ushairi: Shindano la Mashairi litamhitaji Khadim aghani jukwaani tungo zake juu ya mada isemayo "Amani haipatikani bila ya Ahmadiyya" ambapo kibwagizo kitakuwa "Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya"

5. Hadith: Shindano litawataka Khuddam kuhifadhi na kutafsiri Hadithi No.924 na 925 kutoka kitabu cha Kiunga cha watu wema.

Mashindano kwa Atfal:

1. Hifdh-ul-Qur'an (Kuhifadhi Qur'an) Juzuu ya 28, Juzuu ya 29 pamoja na Juzuu ya 30

2. Hadithi: Hadithi 40 + (Maombi ya Mtume s.a.w):-
(i) Dua wakati wa kugutuka baada ya kuona ndoto yenye kutisha (No.4)
(ii) Dua ya kujiongezea elimu (No.7)
(iii) Dua ya kupata ulinzi wa Mwenyezi Mungu (No. 1 - 3)

5. Ushairi kwa Atfal: Atfal watashindana juu ya kughani jukwaani shairi la Masihi Aliyeahidiwa lisemalo 'Muhammad ni nuru' -Mwana Mkuu wa Ibrahim uk.183

NB: Kwa wote; (Khuddam na Atfal), kutakuwepo mashindano ya kuhifadhi maombi ya Mtume (saw) kuanzia dua Na. 1 - 25 kama tulivyoelekeza kwenye kalenda ya Tanzeem.

Pia kutakuwa na mashindano kuhusu sala: Kuhifadhi dua, tahmeed na tasbih za sala pamoja na kupima ufahamu wa maeneo mbalimbali ya sala, pia ufahamu wa aina mbalimbali za sala.

Limetolewa na Muhtamim Ishaat
Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania
Abdillah Kombo (0767 -519497)

Taasisi ya ndoa kwa mwangaza wa mafundisho wa Islam

Kutoka uk. 12

ndoa ndio njia ya kuufikia ucha Mungu na kumlinda mtu dhidi ya upujufu.

Vigezo vya kuchagulia mwenza wa maisha.
Katika kuchagua mwenza wa maisha, ucha Mungu na unyoofu ni lazima vipewe kipaumbele juu ya sifa nyinginezo zote, kama inavyoelezwa na hadithi ifuatayo:-
"Mwanamke huolewa kwa mambo manne; mali yake, ukoo wake, uzuri wake na dini yake. Lakini mnapaswa kumuoa mwanamke mwenye dini, vinginevyo mtapata hasara". (Bukhari Kitabul Nikah).
Hazrat Abu Huraira (ra) anasimulia ya kwamba Mtume Mtukufu (saw) aliulizwa ni yupi mwanamke anayefaa zaidi kuwa mwenza wa maisha? Mtume Mtukufu (saw) alijibu, yule anayemletea furaha mumewe anapomuona na mumewe akimtaka kufanya jambo fulani, anamtii na anaepuka jambo lolote asilolipenda mumewe" (Mishkaat).

Sharti za ndoa (Nikah)
1. Mahar
"Na wapeni wanawake mahari zao kwa hiba". Mahari ni zawadi inayotolewa na muoaji, ambayo hupangwa kabla ya shughuli ya kufunga ndoa. Ni mali ya muolewa. Anaweza kuitumia apendavyo. Hii ni kutambua haki ya mwanamke ya kumiliki mali.

2. Ridhaa ya Muolewa
Sawa na sheria ya Islam, mlezi ni lazima apate ridhaa ya muolewa, na kwa ruhusa ya muolewa ndoa inaweza kufungwa. Walii hana mamlaka ya kumlazimisha msichana kuolewa na yeyote. Sawa na sheria ya Islam, hakuna ndoa bila ya idhini ya muolewa.

3. Mlezi (Walii)
Mlezi humwakilisha muolewa wakati wote wa matayarisho ya ndoa na ufungaji wa ndoa. Kwa istilahi ya Islam mlezi huyu huitwa "Walii". Kwa ajili ya muolewa chaguo la kwanza la mlezi ni baba yake, na asipokuwapo mamlaka huenda kwa kaka na kadhalika.

Faida za ndoa
"Wao ni nguo kwenu na ninyi ni nguo kwao" (2:188)
Hazrat Khalifatul Masih I (ra) anaelezea aya hii kwa kusema, "Allah Mwenye Enzi Anasema kwamba wanawake ni nguo kwenu nanyi ni nguo kwao, kama ambavyo nguo huleta raha, faraja, ulinzi dhidi ya joto, kupendeza, ulinzi dhidi ya maumivu mbalimbali hali ni kama hiyo hiyo kwa wanandoa. Kama ambavyo nguo huleta sitara, hali kadhalika waume na wake wanapaswa kusitiri aibu za mahusiano yao" (Hotba ya ijumaa 4 Juni 1909, Khutbat Nur Pg.400).

Tofauti lakini sawa
Hazrat Ch. Zafrullah Khan (ra) ameandika, "Islam inapinga mtazamo huu, na inamwinua mwanamke na kumweka kwenye daraja la usawa wa kiroho na mwanaume. Inasemwa mwanamume na mwanamke wanategemeana na hii ndio njia ya mafanikio yao wote. Kwa mfano inasemwa "wao ni nguo kwenu nanyi ni nguo kwao" (2:188).

Usawa wa kiroho
Usawa wa kiroho kati ya mwanamke na mwanaume umesisitizwa mara kwa mara katika Qur'an Tukufu. Kwa mfano inasemwa: "Bila shaka wanaume wanaojisalimisha na wanawake wanaojisalimisha, na wanaume wanaoamini na wanawake wanaoamini, na wanaume wanaotii na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa sadaka na wanawake wanaotoa sadaka, na wanaume wanaofunga saumu na wanawake wanaofunga saumu, na wanaume wanaolinda tupu zao na wanawake wanaolinda tupu zao, na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi na wanawake wanaomtaja - Mwenyezi Mungu Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa" (33:36).

"Na Mwenyezi Mungu Awaelekee kwa rehema waaminio wanaume na waaminio wanawake; na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mrehemevu" (33:74)

Baadhi ya miongozo kwa wanaume na wanawake
"Na kaeni nao kwa wema, na kama mkiwachukia basi huenda mchukie kitu na Mwenyezi Mungu Ametia heri nyingi ndani yake" (4:20)

"Mbora wenu ni yule aitendeaye familia yake wema zaidi, nami ni mbora wenu katika kuitendea wema familia yangu" (Miskaat Bab Ashah al Nisa).

Wanaume wanapaswa daima kuzingatia ujumbe mtakatifu "Mbora kati yenu ni yule aitendeaye wema zaidi familia yake".

Halikadhalika wanawake wanapaswa kuwa ni onesho la utii kwa waume zao kwa kuzingatia usemi wa Mtume Mtukufu (saw); "Kama ningeruhusiwa kumwamuru yeyote kumsujudia mwingine minghairi ya Allah, ningeliwaamuru wanawake kuwasujudia waume zao" (Jamii Tirmidhi kitabul Nikah).

Vile vile katika tukio jingine, Mtume Mtukufu (saw) alisema; "Mke anaeiangalia vyema nyumba ya mumewe na kuitunza atapata malipo yale yale ayapatayo mume kwa kutimiza majukumu yake" (Assad al haba).

Mashujaa wa Kalamu

Kutoka uk. 12

Ralph Ellison, James Baldwin, Langston Hughes. Pakistan inamuenzi Mohamed Iqbal, India inamuenzi Tagore na Ujerumani inamuenzi Goethe.

Hakuna maendeleo bila kutazama wenzetu wanafanya nini. Ni kichekesho kwa taifa letu kuwa kisiwa. Imekuwaje tumewasahau kwa haraka waandishi wetu ambao wanawakilisha mapigo na mdundo wa roho ya taifa letu?

Hivyo nilishtuka sana nilipoona waandishi wetu hawakuwekwa kwenye orodha ya mashujaa wa kupewa nishani wakati wa kusherehekea miaka 50 ya uhuru. Tunafanya kosa moja kama taifa, upo wakati kila ukitaja uhuru yule aliyeleta uhuru basi hatajwi mwingine isipokuwa Julius Kambarage Nyerere. Hatuwezi kumnyima nafasi yake katika harkati za uhuru, lakini tukumbuke ya kwamba kidole kimoja hakivunji chawa, kosa lile lile tunalolifanya katika uwanja wa siasa sasa tunaliendeleza katika fasihi. Akitajwa Muandishi basi jina linalojitokeza kwa haraka ni la Shabaani Robert. Hakuna anayeweza kupinga mchango wa Shabaani Robert katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili ila tutakuwa watu wa ajabu tu ambao wana Muandishi mmoja. Na hili linanikumbusha methali moja ya kihaya 'Ekizinakimo kya maruku' - wimbo mmoja wa Maruku. Kila ukiimbwa wimbo unakuwa wimbo ule ule. Je watunzi wa nyimbo wamekwisha? Wakati umefika wa kufanya utafiti na kuwaweka bayana waandishi wetu ili tuepukane na 'Ekizinakimo kya maruku'.

Inatubidi tufanye utafiti na kuwafahamu vilivyo waandishi wafuatao:- Salum Kombo, Khamisi Amani Khamisi Nyamaume, Waziri Kijana, Mwinyihatibu Mohamedi, Mohamedi Ally, Mathias Mnyampala, Mahmood Hamduni Jitukali, Amiri Sudi Andanenga, Sheikh Kaluta Amri Abedi, Ahmad Snowhite, Pala Mlanzi Hassani, Shabani Gonga kwa kuanza na wachache.

Sisi ni taifa huru hatuwezi kuiga kila kitu, lakini yapo yanayofaa ambayo tunaweza kuiga. Katika hili la kuenzi waandishi tufanye uamuzi wa haraka kwani linalowezekana leo lisingoje kesho.

Athari za Ushirikina katika soka

Kutoka uk. 12

yake mizimu ya akina Efford Chabala, Harrison Chongo, Whiteson Changwe, Wisdom Chansa, Moses Chikwalakwala, Eston Mulenga na wenzao ilirudi uwanjani na kusaidia ndugu zao.

Hapa ndipo ushabiki wa soka unapoingia uharamu. Mambo haya huaminiwa hata na watu wanaojinasibu kuwa wafuasi wa dini. Hili ni gonjwa lililoenea dunia nzima, lakini katika Afrika, Amerika ya Kusini na Asia imani hii imefurutu Ada.

Hapa nchini kwetu tatizo la ushirikina katika soka ndilo tatizo linalofanya tupige kwata bila ya kwenda mbele katika soka. Kuna visa vingi vya ushirikina katika soka hasa ihusianapo na pambano la watani wa jadi Simba na Yanga. Kuna hadithi za kurushwa kwa njiwa katika uwanja wa zamani wa taifa, kuna kisa cha wazee wa timu zote mbili kukesha uwanjani wakilinda mipira 'isirogwe'.

Hata hizo kamati ziitwazo za ufundi katika vilabu, hazina uhusiano wowote na taaluma ya mchezo huo, miongoni mwa wajumbe wake hakuna kocha wala mchezaji wa zamani bali aghalabu huundwa na wanaoitwa wazee wa busara ambao kwa kawaida huwa ni wadau wakubwa wa ramli, hirizi, uchawi na uganga wa kienyeji.

Hawa kauli yoyote wanayoitoa huchukuliwa kama ukweli ulioshuka kutoka mbinguni. Wakisema kocha afukuzwe hata akiwa na ujuzi ulioje hazitapita saa 24 atatimuliwa, wakishauri kuwa wachezaji wasipitie mlangoni bali waruke ukuta kama wezi hilo litafanyika bila ya kujali sheria na kanuni za soka wala usalama wa wachezaji hao. Naamini kuna siku watashauri wachezaji waingie uwanjani bila nguo, sina shaka ushauri wao utatiiwa bila maswali.

Kasumba hii chafu ya ushirikina imewakumba hata baadhi ya wachezaji wenyewe. wapo wachezaji wenye 'mafundi' wao wa 'kuwatengeneza' kabla ya kila mechi kubwa. Hii ndiyo siri ya kudorora kwa soka letu na itakuwa ni ndoto za Alinacha kufikiria kuzalisha taifa kubwa la soka tukiwa na imani hizi. Maana hata timu ikishinda pongezi huenda kwa 'wachawi' badala ya Kocha, wachezaji na uongozi wa timu.

Ni lazima tubadilike, tuamini kuwa soka ni mchezo unaotegemea vipaji na taaluma. Timu zote kubwa duniani hazina majopo ya waganga, bali kamati zao za ufundi hujengwa na makocha, wachezaji nyota wa zamani, wataalamu wa afya za michezoni, wanasaikolojia n.k, bali zinao maskauti ambao huhaha dunia nzima kusaka vipaji na pia zina shule na vyuo vikubwa vya mafunzo ya soka. Bila kusahau viwanja vyenye mahitaji yote kwa ajili ya mazoezi ya soka.

Na huku ndiko kuomba Mungu. Ni kweli Mungu Anahusika katika kila kadhia na hivyo si vibaya kufanya maombi mbele ya Mungu ili kutafuta ushindi. Wapo baadhi ya wachezaji ambao hudiriki hata kufunga saumu ya nafali siku moja kabla ya mechi. Kuna tetesi za watu kama Fredrick Kanoute, (Mali) Suleyman Ali Muntari, na Stephan Appiah (Ghana) na hata Nicolas Anelka (Ufaransa) husali na kutoa sadaka misikitini wanapokabiliwa na mechi ngumu. Hawa wawe mfano wa kuigwa hasa kwa wanasoka wa Kiislam.

Islam inafundisha kuwa katika maombi kuna TADBIR na TAQDIR, Tadbir ni jitihadi zote za haki afanyazo mja katika kulitafuta jambo lake, hivyo kuiandaa timu kwa kutafuta wachezaji wenye vipaji vya kweli, kujiandaa kitaaluma, kufanya mazoezi makali ya kimwili ni sehemu moja ya maombi, kisha ukaanguka katika kizingiti cha Mola wako kuomba msaada wake ni sehemu ya hitimisho la maombi.

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) anaelezea maombi kwa kueleza kuwa hata mtu anaposhikwa na maradhi kula dawa ni sehemu ya maombi na hatua inayofuata baada ya kula dawa ndiyo kuomba kudura ya Allah ifanye kazi juu ya dawa ile. Maana Mungu Ameweka uwezo wake wa uponyaji katika dawa hizo, ndiyo maana Mtume (saw) ametufundisha kutaja jina la Mungu lihusianalo na uponyaji wakati wa kunywa dawa. Ametuelekeza kusema 'BISMILLAHI SHAAFI' ndipo tunakula dawa.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Jumadi ul-Awwal 1433 AH | Machi 2012 | Amman 1391 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Mwanamke anaolewa kwa sababu nne: Mali yake, ukoo wake, uzuri wake na dini yake. Basi upate ufaulu kwa kujichagulia mwanamke mwenye dini. (*Bukhari*)

Taasisi ya ndoa kwa mwangaza wa mafundisho wa Islam

Ndoa ni Agizo la Qur'an:
"Na kama mkiogopa kwamba ninyi (kama jamii) mtashindwa kufanya uadilifu katika mambo yahusuyo mayatima baada ya matukio ya vita, basi oeni wanawake wa chaguo lenu ....." (4:4)

Hadithi za Mtume Mtukufu (saw) juu ya ndoa:
Mtume Mtukufu (saw) amesema; "Maisha ya ndoa ndio njia yetu, yule asiyefuata njia yetu si mwenzetu"

"Kuoa ndio matakwa yangu na mwenendo wangu, wale wasiofuata mwenendo wangu si pamoja nami" (Ibne Majah)

"Mtu anapooa amekamilisha nusu nzima ya dini yake" (Mishkaat)

Islam na Useja:
Katika Islam hakuna nafasi ya useja hata kidogo. Maisha bila ndoa yamekatazwa, hata kulaaniwa katika Islam. Imekaririwa katika Sunna Abuu Daud, Mtume Mtukufu Muhammad (saw) amesema kuhusu hili, "Hakuna uruhubani katika Islam".

Lengo la ndoa:
Lengo kuu la ndoa ni kuzaana na kuhifadhi wanadamu, kujilinda na maovu na khulka mbaya na kuunda jamii yenye upendo na amani. Hii ndio sababu Qur'an Tukufu inawaita waliooana muhsan na muhsanah, yaani wale waliolindwa na kuhifadhiwa kama vile wamo katika ngome imara inayolindwa.

Ina maana kwamba mtu anapofunga ndoa, awe mume au mke hupata ulinzi asiuelekee ushetani. Hii ndio sababu, kwa ajili ya ucha Mungu na wema, ndoa ni lazima. Inatoa ulinzi wa hali ya juu dhidi ya maovu na matamanio ya kishetani.

Ndoa inahakikisha kwamba mahitajio ya mwili yanatoshelezwa ndani ya mipaka ya sheria za Mungu. Ikiwa mtu hawezi kumpata mwenza wa maisha yake, anapaswa kufunga saumu. Mtume Mtukufu Muhammad (saw) amesema, "Enyi vijana, yeyote kati yenu anayeweza kuoa na aoe na yeyote asiyeweza kuoa anashauriwa kufunga kwa kuwa kufunga saumu kunapunguza matamanio ya ngono". (*Sahihi Bukhari, kitabu cha Nikkah*).



Masjid Fazal Tabora Tanzania.
(Wenyeji zamani waliuita Taj Mahal ya Tanzania)
Msikiti wa kwanza wa Jamaat Ahmadiyya kujengwa nchini Tanzania (1944).
Sawa na sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w. ndoa hutakiwa kutangazwa msikitini.
Ndoa nyingi za wanajumuiya nchini zimepata baraka hii ya kutangazwa kwenye misikiti yetu.

"Na katika ishara zake ni kuwa Amewaumbieni katika jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao, Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika hayo zimo ishara kwa watu wanaofikiri" (30:22)

Aya hii inamaanisha kwamba ndoa imekusudiwa kuwezesha kupatikana kwa amani ya moyo na mapenzi na maelewano. Allah Amesema pia kwamba

Endelea uk. 11

Athari za Ushirikina katika soka

Ustadhi Abdullah Khamisi Mbanga

Katika dimba la kati, maajabu yalikuwa matamu pia wakati Afisa wa jeshi Chris Katongo alipokuwa akipiga kanzu, chenga na mashuti mbele ya mlinzi mzoefu Habib Kolo Toure. Huwezi kuamini macho yako timu iliyosheheni wanaotukuzwa mno na mashabiki wa soka la Ulaya, kama vile Didier Tito Drogba, Sheikh Tiote, Abduqadir Keita, Grevinho, ikisumbuliwa na vijana wasiojulikana sana wa kizambia kiasi cha kumfanya mlinda mlango wao Abubakar Barry Copa kupata wakati mgumu muda wote wa mchezo.

Kwa ufupi ushindi wa Zambia ulichagizwa mno na moyo wa utaifa (uzalendo), nidhamu na ari kubwa ya kutwaa kombe hilo hasa kwa kukumbusha tukio lililowakuta wakubwa wao miaka 19 iliyopita walipopoteza maisha kwa ajali ya ndege katika Pwani ya Gabon.

Hapandipoitikadizakusikitisha katika soka zilipochafua utamu wote niliyoueleza. Wengi wa mashabiki, kutokana na ile kasumba ya kuthamini mno wanasoka wanaotumika katika soka la Ulaya, hawako tayari kuamini kuwa siku ile Chipolopolo ilikuwa ni maji marefu kwa tembo wa Abidjan bali wanahusisha matokeo ya mchezo ule na imani za kishirikina.

Wanadai kuwa tendo la kwenda kuomboleza katika pwani ile iliyomeza roho za kaka zao kwa ajali ya ndege ilikuwa ni kama kuomba mizimu yao. La kushangaza ni kwamba hata baadhi ya waandishi wa michezo wa magazeti yanayoheshimika kabisa waliandika siku iliyofuata kuwa mizimu ya Zambia yamwandama Drogba, ikiaminiwa pia kuwa hata penati aliyokosa Drogba kwenye dakika ya 70 ya mchezo ilitokana na nguvu za mizimu! La haula! Si Drogba huyu huyu ndiye aliyepoteza penati ya mwisho mwaka 2006 na katika fainali za Cairo? Kule pia walihusisha na nakala za Qurani Tukufu zilizokuwa zimetapakaa uwanjani! Washabiki wa soka kwa ushirikina!

Kwa mtazamo huo wengi wanaamini kuwa siku ile Ivory Coast haikuwa ikicheza na akina Kennedy, Mweene, Chamanga, Katongo, Kalaba wala Mayuka. Bali badala

Endelea uk. 11

Mashujaa wa Kalamu

Na Mahmood Hamsini Mubiru, Dar es Salaam

Mapema mwezi huu, Taifa la Uingereza lilikuwa katika shamra shamra za kumbukumbu ya Muandishi maarufu wa nchi hiyo Charles Dickens ambaye anatambulika duniani kote kama sauti ya wanyonge.

Zilikuwa ni sherehe za kukumbuka mchango wa Mwandishi huyu ambaye kalamu yake imeacha athari za maafa yaliyoletwa na mapinduzi ya viwanda. Kwa kupitia kalamu yake tumeweza kuona ni kwa kiasi gani ubepari ni unyama na ibada kubwa ya mfumo huo ni kupata faida bila kujali njia iliyotumika katika kupata faida hiyo. Ingawaje Charles Dickens aliathiriwa na mazingira ya kwao Uingereza ukweli aliougusa ulivuka mipaka na kuenea mahali pote. Na hiyo ndiyo maana ya uandishi mzuri. Kwani Muandishi mzuri hugusa jambo likavuka mipaka na kuwa mali ya binadamu wote. Ndiyo maana ingawaje tunauchukia sana ukoloni wa Waingereza lakini ni vigumu sana kumchukia Charles Dickens Muandishi yule maarufu.



Bw. Charles Dickens

Muandishi huyu aliwatengeneza wahusika ambao ni vigumu sana kuwasahau. Ukifumba macho unaweza kuona wakitembea na usipoangalia unaweza kuzungumza nao.
Nani ambae hakumbuki kijana Oliver Twist mwenye nguo za matambara, mwenye sura ya huzuni huku amebeba bakuli lake akiomba apewe zaidi? Nani anaweza kumsahau Bwana yule katika Christmas Coral ambaye yeye ana ulafi wa kupitiliza mipaka na hayuko tayari kufungua mikono yake ili kumpatia mtu mwingine riziki.
Ni kweli kuna kila sababu ya kukumbuka kichwa hiki kilichoiletea nchi yake sifa kubwa. Kwa bahati nzuri huu ni utamaduni wa Waingereza, Wamarekaninanchinyingineza Ulaya na Asia. Waingereza kwa mathalani wanamkumbuka kwa mapenzi makubwa na kumuenzi Robert Louis Stevenson ambaye ameacha jina kutokana na riwaya yake ya *'Treasure Island'*. Waingereza hawamtoki mdomoni Bi. Emily Bronte kwa riwaya yake ya *'Wuthering Heights'*. Waandishi wengine wakiwa ni pamoja na Thomas Hardy, George Eliot, George Orwell, D.H. Lawrence, E.M. Forster. Washairi wao maarufu wanazikwa mahala penye heshima na kivutio kikubwa kwa watalii na wale wenye mapenzi na fasihi. Yapo makaburi ya William Shakespeare, John Keats, Lord Tennyson, John Milton, Shelly, Coleridge, Kipling kwa kuwataja baadhi tu.

Nchi nyingine zinazo utamaduni wa kuwaenzi waandishi wao, Marekani inawaenzi Mark Twain,

Endelea uk. 11